SUPA JACKPOT
TZS. 1,142,132,257
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**MADAKTARI** bingwa 60 mifupa, nyonga watua rasmi Arusha

UKURASA 3



**ROBERTINHO NA GAMONDI WAFUNGUKA**

UKURASA 24


# Nipashe

Jumamosi Agosti 12, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581400


www.ippmedia.com

MWANGA WA

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


# OLE WENU, IGP AONYA

UKURASA 2




Mkuu wa Jeshi la Polisi, IGP Camillius Wambura akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kundi la watu linalodai kuandaa na kuratibu maandamano ya nchi nzima yanayodai kulenga kuiangusha serikali ya awamu ya Sita kabla ya mwaka 2025. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

## Prof. Janabi ahadharisha mazoezi bila kupima afya

UKURASA 3

UKURASA WA 2

### SAMIA APANGIA VITUO MABALOZI

RAIS Samia Suluhu Hassan, amewapangia vituo vya kazi mabalozi, wakiwamo wapya sita aliowateua Mei 10, mwaka huu, na...



UKURASA WA 4

### WAGONJWA 10 WAFANYIWA UPASUAJI MKUBWA WA MOYO KUZIBUA MISHIPA

WAGONJWA 10 wamefanyiwa upasuaji mkubwa wa moyo wa kuzibua mishipa ya damu iliyoziba katika kambi...



## Mbowe apokewa na kero huduma za afya

UKURASA 2

MICHEZO GUARDIOLA HATARAJII MAAJABU 2023/24 UK. 22 KATUNI UK. 6



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Gracian Makota akizungumza kwenye kikao cha baraza la madiwani juzi, kuhusu utatuzi wa changamoto na kero za wananchi kupitia bango kitita. Kushoto ni Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Baraka Kanunga. **PICHA: GIFT THADEY.**

# Ole wenu, IGP Wambura aonya

**Beatrice Shayo na Angel Mndolwa**

MKUU wa Jeshi la Polisi Nchini, Inspekta Jenerali (IGP) Camillus Wambura, amewaonya watu au kikundi kinachopanga kufanya maandamano nchi nzima ili kuiangusha serikali kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Ametoa onyo kwamba watu wanaotaka kufanya hivyo, kamwe wasiingie katika mtego huo kwa kuwa watashughulikiwa na dola ipasavyo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, IGP Wambura alisisitiza mtu yeyote asithubutu kuingia katika mtego huo na kama haijui vizuri mamlaka ya vyombo vya dola, safari hii watajua.

Wambura alisema wakati wanatoa taarifa hizo za ajabu (watu hao) wanahusisha maandamano na kushawishi Watanzania kuwaunga mkono na hoja zinazoendelea za uwekezaji wa bandari.

"Tuliamini hoja za bandari hujibiwa kwa hoja na vile vile tuliamini kwa sababu baadhi ya watu hawa walikwenda mahakamani basi wangeheshimu uamuzi wa mahakama badala yake, wametoka na kuanza kutafuta ushawishi na kuchochea kuwataka Watanzania waingie kwenye maandamano ya nchi nzima. "Lakini mmoja amekwenda mbali zaidi akieleza watahakikisha wanaiangusha serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan kabla ya mwaka 2025. Huu ni uhaini. Jambo la kwanza tunawataka watu hawa wakome kabisa na wasitishe matamshi yao," alionya IGP Wambura.

Alisema atakayefanya hivyo atachukuliwa hatua za kisheria kwa uchochezi anaoufanya na uhaini uliopangwa na kwamba hayo ni makosa ya jinai.

Wambura alisema Jeshi la Polisi halitakaa kimya na kuwavumilia kama walidhani liko kimya, basi litawaonyesha kuwa haliko kimya dhidi ya yeyote atakayevunja sheria za nchi. IGP Wambura aliwaomba Watanzania kuwapuuza watu hao kwa kuwa Tanzania ni nchi ya amani, salama na tulivu, hivyo wasikubali kushawishiwa kuiingiza nchi kwenye machafuko.

"Hatujawahi kufika huko na hatutakaa kufika. Kwa hawa wachochezi niwataarifu jeshi letu la polisi ni jeshi imara sana, wasitikise kiberiti. Kama waliwahi kutikisa kwa kipindi cha nyuma wakaguswa wasiende hatua nyingine. Huko wanakoshawishi kwenda ni sehemu mbaya sana. Ninawaonya wasijaribu tena kuendelea kufanya ushawishi na uchochezi huo,"alisisitiza IGP Wambura.

Aliwataka wananchi kuendelea kuwa watulivu na waishi kwa amani na utulivu kama ambavyo ni mazoea, taratibu na desturi za nchi.

IGP Wambura alisema hawakubaliani na aina yoyote ya uhalifu na walitegemea kama kuna mlengo wa kisiasa waende kwenye hoja yasifikie kwenye vitendo vya kihalifu.

"Jeshi tumeona maneno ya kichochezi na ya kutisha yameanza kuibuka na kuweka ushawishi katika jamii zipo hatua zimeanza kuchukuliwa jambo hilo haliwezi kuvumilika,"alisema.

IGP Wambura alisema katika mambo ambayo hayawezi kuvumilika ni ya aina hiyo ya uchochezi na kusema hatua waliyofikia ni mbaya.

# Mbowe apokewa na kero huduma za afya

**Na Aneth Ntungo,** SAUT

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, akiwa katika mwendelezo wa ziara ya +255 visiwa vya Ukerewe mkoani Mwanza, amepokewa na kero mbalimbali ikiwamo ya upatikanaji wa huduma za afya.

Akiwa eneo la Nansio, Mjumbe wa Kamati Tendaji ya CHADEMA Kanda ya Ziwa Victoria, Karoli James, alimweleza Mbowe kwamba huduma za afya visiwani humo hairidhishi, hali inayosababisha baadhi ya wanawake kujifungulia ziwani wakienda maeneo mengine kuzifuata.

"Ukerewe tuna vijiji 75, kata 25 lakini tuna vituo vya afya vinne na zahanati 28. Bado tuna shida kubwa kwenye eneo la afya. Kuna jenereta la hospitali ya wilaya ambalo limenunuliwa kwa Sh. milioni 60 lakini bovu kwa muda mrefu hali inayosababisha watu wanapokuwa kwenye vyumba vya upasuaji kukosa huduma pale umeme unapokatika," alisema. James aliomba serikali iangalie namna ya kuzitatua changamoto hizo kwa kuwapelekea jenereta lingine na kuongeza vituo vya afya kulingana na idadi ya vijiji na watu waliopo huko ili kuokoa maisha ya wajawazito.

Akizungumza katika mkutano huo, Mbowe aliwataka wananchi kusamehe utawala uliopita kwa yote kwa kuwa ulishindwa kuyafanya kwa kile alichokiita kuwa ni tatizo la miongozo ya chama tawala.

Mbowe alisema endapo watakiamini, chama hicho kitahakikisha kinabadilisha mifumo mizima ya utawala ikiwa ni pamoja na kuweka utaratibu wa kusoma mapato na matumizi katika kila kipindi cha utekeleza ili kuweka uwazi wa kila mwananchi kuelewa na kuondoa hali ya ubadhirifu.

Makamu Mwenyekiti wa Chama hicho Bara, Tundu Lissu, aliendelea na mikutano yake katika mikoa ya Mwanza na Mara na kuwapa wananchi elimu kuhusu mkataba baina ya Tanzania na kampuni ya DP World.

Oparesheni ya +255 Katiba Mpya Okoa Bandari kwa awamu ya pili inayoendelea katika mikoa ya Kanda ya Ziwa inatarajia kuhitimishwa leo viwanja vya Furahisha.

# Samia apangia vituo mabalozi

**Na Mary Geofrey**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amewapangia vituo vya kazi mabalozi, wakiwamo wapya sita aliowateua Mei 10, mwaka huu, na kuwabadilisha wengine wanne vituo vya kazi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, Zuhura Yunus, mabalozi wateule wataapishwa Agosti 16, mwaka huu, saa 5:00 asubuhi, Ikulu Chamwino, Dodoma.

Taarifa hiyo iliwataja mabalozi waliopangiwa vituo vya kazi ni Balozi Fatma Mohammed Rajab nchini Oman ambaye anachukua nafasi ya Balozi Abdallah Abbas Kilima ambaye amestaafu.

Balozi Joseph Edward Sokoine amepangwa kuwa Balozi wa Canada, kuchukua nafasi ya Dk. Mpoki Ulisubisya ambaye amestaafu. Mwingine ni Balozi Naimi Sweetie Hamza Aziz, ambaye amepangwa kuwa ubalozi wa Austria.

Aidha, Balozi Mteule Meja Jenerali Ramson Mwaisaka, amepangwa kwenda Rwanda kuchukua nafasi ya Balozi Meja Jenerali Richard Makanzo ambaye amehamishiwa Cairo, Misri.

Taarifa hiyo ilisema Balozi Mteule Gelasius Byakanwa ameteuliwa kwenda Burundi kuchukua nafasi ya Balozi Jilly Maleko ambaye amestaafu. Balozi Mteule Habibu Mohamed amepangwa Kwenda Qatar ambako anachukua nafasi ya Balozi Mahadhi Juma Maalim, ambaye amehamishiwa Kuala Lumpur, Malaysia.

Balozi Mteule Imani Njalikai amepangiwa Algeria kuchukua nafasi ya Balozi Meja Jenerali Jacob Kingu ambaye amestaafu.

Wengine ni Balozi Mteule Hassan Mwamweta aliyepangwa Ujerumani akichukua nafasi ya Balozi Abdallah Saleh Possi, ambaye amehamishiwa Geneva, Uswisi. Balozi Mteule Dk. Mohamed Abdallah (Saudi Arabia) akichukua nafasi ya Balozi Ali Jabir Mwadini, ambaye amehamishiwa Paris, Ufaransa kuchukua nafasi ya Balozi William Shelukindo ambaye aliteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Balozi Meja Jenerali Richard Makanzo amepangwa Kwenda Misri kuchukua nafasi ya Balozi John Emmanuel Nchimbi ambaye anarejea nchini. Balozi John Simbachawene ataiwakilisha Tanzania nchini Uganda akichukua nafasi ya Balozi Aziz Mlima ambaye amestaafu.

"Balozi Abdallah Saleh Possi amepelekwa kuwa Mwakilishi wa Kudumu wa Tanzania katika Ofisi za Umoja wa Mataifa Geneva, Uswisi. Balozi Possi anachukua nafasi ya Balozi Maimuna Tarishi ambaye amemaliza mkataba wake, " ilisema taarifa hiyo.

# Madaktari bingwa 60 mifupa watua rasmi

**Na Allan Isack,** ARUSHA

TIMU ya madaktari bingwa wa mifupa 60 kutoka Marekani, waliwasili jana kwa ajili ya kuanza kutoa huduma bure ya upasuaji wa nyonga na magoti kwa wagonjwa wanaosumbuliwa na maradhi hayo.

Akiwa Uwanja wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), wakati akiwapokea madaktari hao, Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alisema ujio wa madaktari hao ni matokeo ya kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan na serikali.

Dk. Mollel alisema madaktari hao wabobezi watafanya kazi kwa siku saba kwa niaba ya Rais kwa kumgusa kila Mtanzania kwenye utoaji wa huduma bora za afya.

"Ndani ya Tanzania tuna timu mbalimbali ambazo zitazunguka kila sehemu kutoa tiba hii lakini pia baada ya taarifa za ujio huu kusikika, wagonjwa waliojiandikisha wanatoka maeneo mbalimbali ya nchi yetu," alisema Dk. Mollel.

Pia alisema miezi miwili iliyopita alikuwa na Waziri wa zamani wa Maliasili na Utalii, Lazaro Nyalandu, katika Kijiji cha Pohama mkoani Singida ambako madaktari hao walitoa matibabu kwa zaidi ya wananchi 1,500.

"Wako waliotibiwa hapo kijijini na wengine wamechukuliwa kwa ajili ya kuja kufanyiwa upasuaji hapa katika Hospitali ya Seliani jijini Arusha," alisema.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Seliani, Dk. Goodwill Kivuyo, alisema amefurahia kuwapokea wageni hao maalum wa Rais Samia kwa kuwa magonjwa ya nyonga na mifupa yamekuwa tatizo kubwa linalowasumbua watu wengi.

"Katika hospitali wagonjwa wengi ni wa mifupa na wagonjwa wanaokwenda katika kiliniki wanakabiliwa na tatizo la nyonga na magoti.


"Ujio wa madaktari hawa utakuwa jambo kubwa kwa wagonjwa wetu kupata huduma hii kwa kuwa gharama ya upasuaji huu kwa hapa nchi hasa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili ni takribani zaidi ya Sh. milioni 28," alisema.

Dk. Kivuyo alisema madaktari hao ni wabobezi katika kada hiyo na watatoa huduma za matibabu bure na itakuwa faida kwa walengwa. Mratibu wa Shughuli hiyo, Nyalandu, alisema kutolewa kwa huduma hiyo ni maelekezo mahususi ya Rais Samia ya kuendelea kutoa huduma bora za matibabu hasa kwa kanda zote. Pia alisema wamewashauri wadau hao ikiwezekana wafike na kwenye mikoa ya Mtwara, Lindi, Iringa, Mbeya, Njombe, Kigoma, Tabora, Mwanza Shinyanga, Singida, Dodoma na maeneo mengine.

"Mimi kama mratibu, ninaamini azma ya Mheshimiwa Rais Samia itafanikiwa. Pia tunatarajia watu wa kaskazini mwa Tanzania na maeneo mengine ya nchi yetu wataona upendo wa mama kwa kuwashika mkono watu ambao kwa hali ya kawaida wasingeweza kusaidia," alisema Nyalandu.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongela, alisema serikali imewekeza kwenye elimu na afya za Watanzania, hivyo aliwakaribisha wananchi kwenda kupatiwa huduma.

"Kundi hili la madaktari limekuja kutoa huduma za kimatibabu kwa Watanzania na kuwapa furaha na amani kwa kuwa ndiyo lengo kubwa la Mkuu wa Nchi. Pia huu ni uthibitisho wa uhusiano ulioko kati ya nchi yetu na mataifa mengine duniani, kama mteule wa Rais ninaahidi serikali ya Mkoa wa Arusha itatoa ushirikiano wa kutosha wakati wa shughuli hii inapofanyika," aliahidi.0




Waziri wa Nishati, January Makamba (kulia) na Waziri wa Nishati wa Malawi, Ibrahim Matola, wakibadilishana hati jijini Dar es Salaam jana, baada ya kutiliana saini mkataba wa makubaliano ya kuzalisha umeme katika Mto Songwe. Habari Uk. 4. **PICHA: MIRAJI MSALA.**

# Janabi ahadharisha mazoezi bila kupima afya

**Na Beatrice Shayo**

MKURUGENZI Mtendaji Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Prof. Mohamed Janabi, amesema wanaofanya mazoezi ya kukimbia, maarufu kama 'jogging, wako katika hatari ya kuanguka na kupoteza maisha gafla.

Prof. Janabi aliyasema hayo juzi jijini Dodoma wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa majukumu na mwelekeo wa utekelezaji wa majukumu kwa mwaka 2023/24.

Alisema mauti inaweza kuwakuta watu wa aina hiyo kama ambavyo inavyotokea kwenye viwanja vya mpira iwapo watakuwa hawajatambua afya hasa wale wenye ugonjwa wa moyo. Prof. Janabi aliwaomba waandishi wa habari wasiangalie tu wachezaji kuanguka uwanjani.

"Siku hizi kuna 'j'ogging' kila mahali nimeona. Ningeomba watu wapime afya zao kwa sababu wale wanaoanguka mpirani na huko 'jogging' utaanguka vivyo hivyo,"alisema.

Alikumbushia akiwa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), michuano ya Kombe la Mataifa la Afrika (AFCON) iliyofanyika Cairo, Misri Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) lilipeleka timu ya taifa kufanyiwa uchunguzi na kwamba wachezaji wawili waliondolewa kwa sababu walionekana wanaweza kuanguka uwanjani halafu wakadhani wamelogwa.

Watu hao, alisema walikuwa na matatizo ya moyo kuwa mikubwa na kusema mtu akiwa na tatizo hilo anaweza kuanguka kiwanjani ghafla na kupoteza maisha.

"Wakati nipo mdogo alianguka mchezaji wa Simba na kufariki dunia, anaitwa Hussein Tindwa. Walisema huyo amerushiwa kitu, hakuna alichorushiwa tatizo ni moyo. Jogging ama GYM (eneo la kufanya mazoezi ya viungo) ni kitu kizuri jambo la msingi ni kupima moyo kabla ya kuingia katika mazoezini. "Ninashukuru kwa TFF, sijui vyama vingine vya michezo na Baraza la Michezo wanatakiwa kuangalia watu wote wa michezo hasa hii michezo inayotumia nguvu ni muhimu kufanya uchunguzi na hivi vilabu vyetu vikubwa unaingiaje gharama kubwa hujui afya ya mchezaji utalipa mamilioni atakuja siku mbili anakutwa na tatizo la moyo.

"Na jogging tunatakiwa kupima afya zetu, huu ugonjwa unaweza kukukuta upo katika mazoezi," alisema Prof. Janabi.

Alisema JKCI ina vifaa kamili ya kukagua wachezaji na Hospitali ya Muhimbili imethibitishwa.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
12.08.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Jumanne tarehe **15-08-2023** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port kuelekea Rufiji,** gari hizo zina namba za usajili: **T 641 DFA / T 877 EAU T 289 EDD / T 394 DVS**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:

**Urefu** - **mita 20.40**
**Upana** - **mita 4.20**
**Kimo** - **mita 4.60**

2. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam, Pwani hadi Rufiji kupitia Kibiti,** gari zitasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

# Wagonjwa 10 wafanyiwa upasuaji mkubwa wa moyo kuzibua mishipa

**Na Joseph Mwendapole**

WAGONJWA 10 wamefanyiwa upasuaji mkubwa wa moyo wa kuzibua mishipa ya damu iliyoziba katika kambi maalumu ya matibabu ya moyo ya siku saba.

Kambi hiyo iliyomalizika jana katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) , jijini Dar es Salaam, imefanywa na madaktari bingwa wa upasuaji wa moyo na mishipa ya damu wa JKCI kwa kushirikiana na wenzao kutoka Hospitali ya Max ya India.

Mkurugenzi wa Upasuaji wa JKCI, Dk Angela Muhozya, alisema kambi hiyo imefanyika kwa mara ya nne kwa kushirikiana na wataalam kutoka Hospitali ya Max kwa kuwafanyia upasuaji wagonjwa waliohitaji utaalamu zaidi kutokana na mioyo yao kuwa na uwezo mdogo wa kufanya kazi.

Dk. Muhozya alisema kambi hiyo ililenga kufanya upasuaji mkubwa wa moyo kwa watu wazima ambao wana mishipa ya moyo iliyoziba lakini pia viwango vya ufanyaji kazi wa mioyo yao kuwa chini ya asilimia 30.

"Upasuaji ambao tumewafanyia wagonjwa hawa ni mgumu kidogo. Tumekuwa tukiwafanyia uchunguzi wagonjwa hawa na kuwakaribisha wenzetu kutoka Hospitali ya Max ili kwa pamoja kuwahudumia wagonjwa hawa lakini pia kuongeza ujuzi wetu katika kuwahudumia wagonjwa wa aina hii", alisema.

"Katika kambi hii wagonjwa wamepandikizwa mishipa ya moyo mitatu na wengine zaidi ya mitatu bila ya kuusimamisha moyo kwa mafanikio makubwa hii kwetu sisi ni hatua kubwa katika kutoa huduma kwa wagonjwa wa moyo", aliongeza.

Dk. Muhozya pia alisema JKCI inatarajia kufanya upasuaji wa mshipa mkubwa wa moyo ambao umetanuka, kubadilisha mishipa ya moyo pamoja na kuweka mlango mpya kwa wagonjwa ambao wana matatizo ya mishipa mikubwa ya moyo kutanuka.

Naye daktari bingwa wa upasuaji wa moyo na mishipa ya damu kutoka Hospitali ya Max, Subhash Sinha, alisema ushirikiano wake na wataalam wa JKCI unaonyesha mafanikio makubwa tangu walipoanza kushirikiana hadi sasa.

Dk. Sinha alisema kupitia upasuaji wa moyo ambao amekuwa akifanya na wataalam wa JKCI amekuwa pia akitoa mafunzo na mbinu mbalimbali za kufanya upasuaji mkubwa wa mishipa ya moyo kwa wagonjwa ambao mapigo yao ya moyo yapo chini ya asilimia 30 bila ya kuusimamisha moyo.

"Ujio wangu hapa JKCI kwa kawaida huwa ni wa wiki moja, naamini hizi wiki moja moja ninazokuja kuwasaidia wagonjwa kupata matibabu wataalam wa JKCI nao hupata nafasi ya kujifunza kwani sasa naona mabadiliko makubwa wakati tunafanya upasuaji", alisema Dk. Sinha.

Dk. Sinha alisema anatamani siku moja JKCI iwe taasisi kubwa Afrika inayotegemewa na wagonjwa wa moyo walioopo Afrika kwani gharama za matibabu ni zakawaida tofauti na zile zinazotolewa nje ya Afrika lakini pia uwekezaji wa vifaa tiba vilivyopo katika Taasisi hiyo vinajitosheleza kutoa huduma za kibingwa za matibabu ya moyo.




Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dk. Benson Ndiege akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, kuhusu utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya tume hiyo na mwelekeo wa mwaka wa fedha 2023/24. **PICHA: PAUL MABEJA**

# TCDC yavunja bodi 55 vyama vya ushirika

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

TUME ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) imezivunja bodi 55 za vyama vya ushirika kutokana na kuwapo kwa upungufu wa kiutendaji kwenye uandishi wa vitabu, urasimishaji wa mali za vyama, utunzaji wa nyaraka na kumbukumbu.

Upungufu mwingine wa kiutendaji ni madeni ya muda mrefu katika taasisi za kifedha na uzingatiaji wa miongozo ya Mrajis.

Mtendaji Mkuu wa Tume hiyo na Mrajis wa Vyama vya Ushirika Tanzania, Dk. Benson Ndiege, alisema hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa majukumu mbalimbali na mwelekeo wa mwaka wa fedha 2023/24.

"Hatua zilizochukuliwa kwa vyama vya ushirika ni kuvunja bodi 55 za vyama vya ushirika, kupeleka masuala 30 polisi na masuala 47 yanashughulikiwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU). Tume imetoa mafunzo kwa watendaji 4,732 wa vyama vya ushirika kuhusu uandishi wa vitabu na viongozi wa vyama wametakiwa kujieleza," alisema Dk. Ndiege.

Alisema katika mwaka wa fedha uliopita, tume ilifanya ukaguzi wa mara kwa mara katika vyama hivyo ili kubaini uzingatiwaji wa matakwa ya sheria, kanuni na miongozo mbalimbali inayohusiana na utendaji wao.

"Katika kipindi cha mwaka 2022/23 hadi kufikia Juni, mwaka huu, TCDC ilifanya ukaguzi wa jumla ya vyama vya ushirika 4,712 kati ya vyama 7,300 vya ushirika kupitia Ofisi ya Tume Makao Makuu na Ofisi za Warajis Wasaidizi wa Mikoa,"alisema.

Dk. Ndiege alisema matokeo ya ukaguzi huo yalionyesha kuwapo kwa upungufu katika utendaji wa vyama vya ushirika hususani maeneo ya uandishi wa vitabu, urasimishaji wa mali za vyama, utunzaji wa nyaraka na kumbukumbu nyingine za vyama, uzingatiaji wa miongozo ya Mrajis, na madeni ya muda mrefu katika taasisi za kifedha.

"Jitihada zinazotekelezwa na Tume kwa kushirikiana na COASCO, Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU) na wadau hadi kufikia Juni, 2023 maofisa ushirika kutoka mikoa 16 ya Tanzania Bara walipatiwa mafunzo ya ukaguzi na usimamizi wa vyama," alisema.

Alisema mikoa hiyo ni Mtwara, Lindi, Ruvuma, Njombe, Iringa, Tabora, Shinyanga, Mwanza, Kagera, Mara, Kigoma, Simiyu na Geita, Morogoro, Pwani na Dar es Salaam.

Kadhalika alisema Tume imeendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa maofisa hao kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa vyama.

"Katika mwaka 2022/2023 hadi kufikia mwezi Machi 2023, Tume ilinunua kompyuta 226, viti 70, magari 12 na pikipiki 147, Tume imepokea magari matatu kutoka Wizara ya Fedha na gari moja kutoka taasisi isiyo ya kiserikali kwa ajili ya ofisi za mikoa," alisema.

Alisema hadi kufikia mwaka 2022/2023, Warajis Wasaidizi wa mikoa 20, wamepatiwa magari na mikoa sita bado haijapatiwa magari.

Pia alisema tume kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) imetengeneza Mfumo wa Kidigitali wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU), unaolenga kurahisisha usimamizi na uendeshaji wa vyama vya ushirika kwa nia ya kuongeza ufanisi, uwazi na uwajibikaji. "Sambamba na kuboresha utendaji, mfumo huu unasaidia kupunguza gharama za uendeshaji, kuwa na uhakika wa kupata takwimu na kuimarisha utendaji na uendeshaji wa vyama. Hadi kufikia Juni 2023, vyama vya ushirika 5,424 kati 7,300 vimesajiliwa katika Mfumo wa kidigitali wa MUVU,"alisema.

Dk. Ndiege alisema kwa kushirikiana na wizara na taasisi zinazosimamia uendeshaji wa elimu zinafanyia kazi uwezekano wa kuingiza elimu ya ushirika katika mitaala ya elimu ya msingi na sekondari.

# Tanzania, Malawi kuzalisha MW 180 za umeme Songwe

**Restuta James na Elizabeth Zaya**

MAWAZIRI wa Tanzania na Malawi, wametia saini makubaliano ya ushirikiano ya uzalishaji nishati katika maeneo matatu ikiwamo kuzalisha umeme kwa pamoja wa megawati 180 katika Mto Songwe.

Maeneo mengine ya ushirikiano wameyataja ni utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi na ujenzi wa miundombinu kusafirisha umeme.

Makubaliano hayo yalitiwa saini jana Dar es Salaam kati ya Waziri wa Nishati, January Makamba na Waziri wa Nishati wa Malawi, Ibrahim Matola na kuhudhuriwa na wakurugenzi kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA).

Akizungumza baada ya utiaji saini, Makamba alisema ufuatiliaji na utekelezaji wa makubaliano hayo utafanywa na kamati ya wataalam itakayoshirikisha wajumbe kutoka nchi zote mbili.

Waziri Makamba alisema vikao rasmi kwa utekelezaji huo vitaanza Oktoba, mwaka huu na kwamba mapendekezo ya wataalam ndiyo yatatoa mwelekeo wa namna bora ya kutekeleza makubaliano hayo.

"Haya ni matokeo ya ziara na maelekezo ya marais wetu walizozifanya na kuona kwamba kuna umuhimu wa nchi zetu kupanua maeneo ya ushirikiano na mojawapo likiwa ni nishati," alisema Makamba.

Alisema makubaliano hayo ni kati ya serikali za nchi hizo pamoja na mashirika yake yanayoshughulika na nishati.

Makamba alisema makubaliano hayo ni mwendelezo wa utekelezaji wa maamizio ya Marais wa Afrika ya kuzalisha nishati ya kutosha na kuunganisha gridi za taifa za nchi zao.

Waziri Matola alisema makubaliano hayo yanalenga kutekeleza malengo ya milenia ya 2030 ya kuhakikisha wananchi wanapata nishati safi ya uhakika na kwa gharama nafuu.

Alisema umeme utakaozalishwa karika Mto Songwe utagawanywa kwa usawa kwa nchi hizo mbili na kwamba utasaidia kuboresha huduma za kijamii kwa wananchi wa Malawi hususani elimu na afya.

"Tutaboresha njia kuu ya kusafirisha umeme kutoka Mji Mkuu wa Lilongwe mpaka unapojengwa mradi na tumeupokea kwa mikono miwili," alisema Matola.

HABARI KITAIFA

# NEC yataka wasimamizi wenye uwezo

**Na Renatha Msungu**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imewataka wasimamizi wa uchaguzi kutekeleza wajibu wao kwa kuhakikisha ajira za watendaji wa uchaguzi zinazingatia sifa na uwezo.

Makamu Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji Mstaafu wa Mahakama ya Rufani Mbarouk Salim Mbarouk, alisema hayo jana mjini hapa wakati akifunga mafunzo kwa wasimamizi wa uchaguzi, wasimamizi wasaidizi na maofisa uchaguzi.

Mafunzo hayo ya siku tatu yalihudhuriwa na washiriki 88 kwa lengo la kufanya maandalizi ya uchaguzi mdogo wa Jimbo la Mbarali na kata sita za Tanzania Bara.

"Tuna imani kuwa mtateua na kuajiri watendaji wenye sifa na uwezo wa kufanya kazi hii muhimu, jambo hili limekuwa likisisitizwa tokea siku ya kwanza ya mafunzo kwa kuwa hao ndio watakaosimamia mchakato wa kupiga kura na kuhesabu kura vituoni, kazi ambayo inahitaji umahiri, umakini na weledi katika kuitekeleza,"

alisema Jaji Mbarouk.

Jaji Mbarouk alisisitiza kuhusu kuhakikisha kwamba mafunzo kwa watendaji wa vituo vya kupigia kura yanafanywa kwa ufanisi ili wawe na uelewa na kuweza kufanya kazi zao kwa usahihi na kujiamini.

"Ni imani yetu kuwa mafunzo ya watendaji wa vituo yatafanyika kwa ufanisi na weledi katika tarehe zilizopangwa kwenye ratiba ya utekelezaji wa shughuli za uchaguzi.

"Mafunzo hayo yanalenga kuwajengea uwezo ili waweze kufahamu majukumu yenu na kuyatekeleza ipasavyo wakati wa uchaguzi," alisema Jaji Mbarouk.

Pia aliwahimiza watendaji wa uchaguzi kutenga muda kujisomea ili kupata ufahamu wa sheria, kanuni na maelekezo mbalimbali yanayotolewa na tume.

"Ninatumia nafasi hii kuendelea kuwasisitiza kuhusu umuhimu wa kutenga sehemu ya muda wenu kusoma katiba, sheria na maelekezo mbalimbali yanayotolewa na Tume ili yawaongoze katika kusimamia uchaguzi utakaokuwa huru na wa haki," alisema.

Uchaguzi mdogo wa Jimbo la Mbarali na kata sita za Tanzania Bara unatarajia kufanyika Septemba 19, mwaka huu.




Kamanda wa Polisi wa mkoa wa Iringa, Allan Bukumbi akionyesha kwa waandishi wa habari jana, bunduki aina ya gobole iliyotengenezwa kienyeji iliyokamatwa katika oparesheni ya jeshi hilo, mkoani humo. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Wafanyabiashara wagomea tozo mpya za usafirishaji wa samaki

**Na Aneth Ntungo,** SAUT

WAFANYABIASHARA katika soko la samaki la Kirumba, Manispaa ya Ilemela jijini Mwanza, wamegoma wakishinikiza kuondolewa ongezeko la tozo za usafirishaji wa samaki na mazao yake iliyoongezeka ghafla kutoka Sh. 10 hadi Sh. 100 kwa kila kilo moja.

Wakizungumza na Nipashe juzi kwa nyakati, tofauti wafanyabiashara wa soko hilo walisema ushuru wa kibali umepanda kwa kiasi kikubwa sawa na ongezeko la Sh. 90,000 kwa tani moja, hivyo kusababisha biashara hiyo kuwa ngumu.

Tozo hizo, walisema ni kubwa kulinganisha na mitaji yao na kuiomba serikali izipunguze ili waweze kufanya biashara kama ilivyokuwa awali.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, James Katembo, alisema sababu ya kugoma kuendelea na shughuli zao za biashara ni kutokana na serikali kuweka tozo hizo bila kuwashirikisha na kujua hali zao kibiashara.

"Ushuru wa kibali umepanda kutoka Sh. 10 mpaka Sh. 100 hapo bado kuna ushuru wa halmashauri ambao ni Sh. 525,000 kwa tani sawa na kilo 75. Bado hapo hapo mtu anatakiwa kulipia Sh. 70,000 kwa ajili ya upimaji wa sampuli sasa kwa tozo hizi biashara tunafanyaje?" alihoji Katembo.

Mfanyabiashara mwingine, Mafwele Nagabona, alisema kupanda kwa tozo hizo kumesababisha wanunuzi kutoka nje kununua bidhaa hizo moja kwa moja kutoka kwa wavuvi hali inayosababisha biashara kuwa ngumu. Ofisa Uvuvi wa Manispaa ya Ilemela, Humphrey Tillya, akizungumza na wafanyabiashara hao, alisema utaratibu wa ongezeko la tozo hizo umetoka wizarani na wao wanafanya utekelezaji.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, Kiomoni Kibamba, aliwataka wafanyabiashara katika soko hilo kuwa wavumilivu na kuendelea na biashara kama kawaida wakati wanaendelea kulishughulikia suala hilo.

# Tani 5,350 mbaazi zakusanywa 2023/24

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

Chama Kikuu cha Ushirika cha Wakulima Tunduru (TANCU) mkoani Ruvuma kimekadiria kukusanya tani 5,350 katika msimu wa 2023/24.

Meneja wa Shughuli za chama hicho, Marcelino Mrope, alisema hayo juzi wakati akizungumza na wadau wa mkutano wa maandalizi ya msimu wa mauzo ya mbaazi kwa mwaka 2023/24 uliofanyika katika ukumbi wa Clasta ya Walimu wa Tarafa ya Mlingoti, mjini hapa.

Mrope alisema msimu wa mwaka 2022/23 walikusanya mbaazi tani 3,035 ambazo ziliuzwa katika minada sita huku bei ya juu ikiwa Sh. 1,020 na chini ikiwa Sh. 798 sawa na bei wastani ya Sh. 898.25 ambayo ilikuwa ndogo ikilinganishwa na bei ya Sh. 1,2640 iliyotolewa katika msimu wa mwaka 2021/22.

Kuhusu mfumo wa stakabadhi mazao ghalani, Meneja Mkuu wa Chama Kikuu cha Ushirika Tunduru (TAMCU), Imani Kalembo, alisema mfumo huo una manufaa makubwa kwa wakulima ikilinganishwa na mfumo huria.

Alisema kupitia mfumo huo, wakulima wanapata fedha zao zikiwa salama kupitia akaunti ya benki tofauti na mfumo huria ambao ni hatarishi kutokana na kushamiri kwa matukio ya ujambazi.

Kwa mujibu wa Kalembo, mafanikio mengine ni pamoja na serikali kuwa na takwimu sahihi za uzalishaji pamoja kupata ushuru.

Akizungumzia upatikanaji wa vifungashio, Kalembo alisema tayari kimekwishaleta viroba 145,000 vyenye uwezo wa kukusanya kilo 7,250,000.

Akitoa salamu za serikali, Mkuu wa Wilaya ya Tunduru, Julius Mtatiro, aliwataka viongozi wa vyama vya ushirika vya msingi (AMCOS) kusimamia ipasavyo ubora na usafi wa zao hilo wakati wa ukusanyaji ili kuvutia wanunuzi.

Aidha, Mtatiro alimtaka mkurungenzi mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru kuanzisha vikosi kazi ambavyo vitasaidia kudhibiti utoroshaji wa mazao na kwenda kuyauza katika wilaya jirani za Nachingwea mkoani Lindi na Nanyumbu mkoani Mtwara.

Akifunga mkutano huo makamu Mwenyekiti wa TAMCU, Pino Chipojola alihimiza uaminifu na uadilifu wa mali za wakulima ili kuwafanya waendeleze imani kwa vyama vyao.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Simba SC, Yanga onyesheni ufundi, ubora msimu mpya

**WATANI** wa jadi nchini, Simba na Yanga zote kutoka Dar es Salaam zinatarajia kukutana katika mechi ya hatua ya fainali ya mashindano ya Ngao ya Jamii itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini, Tanga.

Yanga ndio mabingwa watetezi wa taji hilo na imefanikiwa kufika hatua hiyo baada ya kuwafunga Azam FC mabao 2-0 wakati Simba ililazimika kwenda katika matuta baada ya kutoka sare ya bila kufungana ndani ya dakika 90 za kawaida.

Simba ilitinga fainali hiyo ya kwanza baada ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kubadilisha mfumo wa shindano hilo kwa kuifunga Singida Fountain Gate FC penalti 4-2.

Kabla ya mechi hiyo ya fainali itakayofanyika kuanzia saa 1:00 usiku, Azam itashuka dimbani kuwakabili Singida Fountain Gate katika mchezo wa kusaka mshindi wa tatu, mechi hiyo pia ikichezwa kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani.

Mechi zote hizo zinachezwa kama ishara ya ufunguzi wa msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambao rasmi utaanza Jumanne kwa timu sita kushuka dimbani kuwania pointi tatu muhimu.

Kuelekea fainali hiyo ya Ngao ya Jamii, mashabiki na wadau wa kandanda kutoka ndani na nje ya Tanzania wanatarajia kuona burudani safi kutoka timu zote mbili, na hii inatokana na kila upande kufanya maandalizi mazuri.

Simba na Yanga zimefanya usajili wa wachezaji wenye viwango na uzoefu wa kucheza mechi mbalimbali za mashindano, makocha wakiboresha vikosi baada ya kufanya tathmini ya kiufundi kutokana na ripoti ya msimu uliomalizika.

Kwa kuangalia msingi huo, mashabiki, wanachama na wadau wa soka wanasubiri kuona wachezaji wakicheza soka la kuvutia na la kiufundi kwa sababu ya maandalizi sahihi ambayo vikosi vyote vimefanya, na kila upande ukisema malengo yao ya kufanya vyema.

Mechi hii si tu inafungua msimu mpya, lakini ni mchezo ambao unaweza kuonyesha ukubwa na mwanga wa kila timu kuelekea katika mbio za kuwania taji la Ligi Kuu Tanzania Bara, Kombe la FA na mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ambayo vigogo hao watachuana.

Wachezaji wanatakiwa kufahamu kujituma na kucheza kwa bidii katika dabi hiyo, si tu kutaipa timu yake matokeo chanya na taji la kwanza kwa msimu wa mwaka 2023/2024, lakini pia kutawaweka katika nafasi nzuri ya kujitanganza kwa mawakala na makocha wa klabu nyingine kubwa za nje ya Tanzania.

Dabi ya Simba na Yanga ni moja ya michezo inayofuatiliwa zaidi kutokana na umaarufu wake, hivyo wachezaji wakumbuke hilo kwao ni daraja kubwa na soko la kujitangaza, vile vile itawasaidia kupata namba katika vikosi vya timu zao za taifa kwa sababu makocha wote wenye wachezaji hufuatilia mechi hiyo.

Tunawakumbusha wachezaji kucheza kwa nidhamu wakati wote wa mechi, kila mmoja anatakiwa kuyafahamu na kuyatekeleza majukumu yake ili timu ifikie malengo na si vinginevyo.

Pia tunawakumbusha wachezaji kuepuka majibishano yasiyokuwa na msingi na mwamuzi lakini pia kufanyiana faulo ambazo zinaweza kumwondoa mwenzako ndani ya uwanja katika kipindi kirefu hali ya kuwa utimamu wa kila mmoja ndio jambo linalohitajika.

Nipashe inawataka waamuzi ambao watapata dhamana ya kuchezesha mchezo huo kuonyesha 'Fair Play' ambayo itasaidia timu inayostahili kushinda kupata taji hilo.

Lakini Nipashe inawataka mashabiki wa soka watakaofika kwenye Uwanja wa Mkwakwani kuonyesha nidhamu kwa kukubaliana viwango vya wachezaji na waamuzi vitakavyoonyeshwa katika mtanange huo na kuacha kuingia uwanjani wakiwa na matokeo yao mfukoni.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

### Waamuzi watende haki na kuwalinda wachezaji



Na Adam Fungamwango

**KIVUMBI** kinatarajiwa kutimka kesho kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani, Tanga wakati miamba ya soka Tanzania Bara, Simba na Yanga zitakapopambana kuwania Ngao ya Jamii ikiwa ni ishara ya kuanza kwa msimu mpya wa mwaka 2023/2024.

Pambano hilo linasubiriwa na idadi kubwa ya wadau wa soka wa ndani na nje ya Tanzania kwa sababu linabeba hisia za mashabiki wengi kutokana na historia ya klabu hizo mbili.

Zinapocheza Simba na Yanga nchi husimama kwa dakika 90, kwani watu wengi mashabiki na hata wale ambao si wapenzi sana wa soka wanasimamisha shughuli zao, au hata wakiendelea lakini macho na masikio yanakuwa katika mechi hiyo.

Mechi ya kesho itaingia kwenye rekodi kwani itachezwa kwenye Uwanja wa Mkwakwani na kuwa moja ya mapambano machache kuchezwa nje ya Dar es Salaam, lakini pia hakuna rekodi sahihi inayoonyesha vigogo hao waliwahi kucheza Tanga.

Rai yangu ni kwa waamuzi wote wa mechi hiyo kuwa waangalifu ili wasizungumziwe zaidi wao badala ya mchezo wenyewe na wachezaji baada ya pambano hilo kumalizika.

Kwa asili ya mechi hiyo waamuzi wanatakiwa kuongeza umakini katika kila tukio, ikiwa ni pamoja na kuchezesha kwa haki, bila kupendelea upande wowote, wala kusawazisha mambo.

Kikubwa waamuzi wanatakiwa waiache mechi hiyo ijichezeshe yenyewe na siyo wao kulazimisha mambo.

Mara nyingi katika mechi hizo unaweza kukuta wachezaji wanacheza kawaida, lakini waamuzi ndiyo wanakuwa na presha kuliko wao au mashabiki walioko majukwaani au kwenye televisheni. Ni mechi inayotakiwa ichezeshwe na waamuzi ambao si waoga kutoa maamuzi muda wowote na mahali popote ili mradi tu tukio limefanyika na yeye ana uhakika na hilo.

Tumeshuhudia waamuzi wakiogopa kufanya maamuzi kwenye mechi kama hizo mwanzo kabisa, lakini linatokea tukio kama hilo baadaye anashindwa tena kuamua makusudi akihofia kwa sababu mwanzoni aliacha tukio la aina hiyo.

Katika hali ambayo si ya kawaida nimeanza kuona baadhi ya wachezaji katika mechi kadhaa wakicheza rafu mbaya na za makusudi huku waamuzi wakishindwa kuchukua hatua stahiki.

Hili limeanza kuwa tatizo sugu kwenye soka letu la Tanzania, wachezaji wamekuwa hawalindani, huku waamuzi nao wakishindwa kuwalinda badala yake mechi ya soka muda wote inakuwa kama mchezo 'rugby'.

Yaani mchezaji anaamua kwa makusudi kumchezea rafu mwenzake akijua kabisa hawezi kuadhibiwa kwa kiasi cha faulo aliyocheza.

Nadhani baadhi ya wachezaji Tanzania wameshajua waamuzi wamekosa mamlaka uwanjani, ndiyo maana unaweza kuona mchezaji anacheza faulo, halafu huyo huyo anakwenda kumbwatukia mwamuzi, anamsukuma na hapati kadi yoyote ile.

Binafsi ningependa mechi ya kesho ichezeshwe na waamuzi wenye uthubutu, majasiri, wenye mamlaka na kutowavumilia wachezaji watovu wa nidhamu bila kuhofia nani au kina nani watasema nini ili mradi tu yupo ndani ya sheria na kanuni za soka.

Ningependa waamuzi wawalinde wachezaji wa timu zote mbili kwani kunakuwa na baadhi ya matukio ambayo si ya kiungwana na wanashindwa kuyachukulia maamuzi kwa woga tu.

Moja kati ya kutokuwa na sifa ya mwamuzi bora ni woga kwa sabau haina tofauti na hakimu.

Tunawatakia waamuzi wote wa mechi ya kesho uchezeshaji mwema usiokuwa na woga wala upendeleo, huku wachezaji pia kuacha kuumizana kwa makusudi kwa sababu wanajua mpira ndio kazi yao kuu inayowaingia kipato.

Mashabiki wanataka mechi ikiisha kila mmoja anasifia uchezaji bora wa timu yake na wachezaji wao, hivyo wanatakiwa kutandaza soka safi na si kucheza rafu zisizo na mpango.

# Waziri ataja mikakati kumaliza migogoro ardhi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, amesema hadi sasa nchi imepimwa kwa asilimia 25 tu na ndiyo sababu ya kuwapo kwa migogoro mingi ya ardhi.

Kutokana na hali hiyo, serikali inatarajia kuzalisha ramani za msingi na uzinduzi wa kituo unaotarajiwa kufanyika Septemba 8, mwaka huu, ambazo zitasaidia kuongeza kasi ya upimaji ardhi.

Dk. Mabula aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya kumaliza mchakato wa ugawaji wa hati kwa wananchi wilayani Makete mkoani hapa ambapo kati ya wamiliki 88 wa ardhi waliojitokeza na kukabidhiwa ni 25 tu.

"Tumepewa fedha ya kutosha Sh. bilioni 345 kwa ajili ya kuboresha mifumo lakini kuweka alama za upimaji. Tuna Sh. milioni 65 ambazo zimetolewa na Benki ya Exim ambazo nazo zinakwenda kuboresha habari nzima ya upimaji.

"Katika kupima lazima uwe na ramani ya msingi na hatukuwa na uwezo wa kuzalisha ramani za msingi lakini kwa sasa tutakwenda kuzalisha ramani zetu na bahati nzuri kituo kile kitakwenda kuzinduliwa Septemba 8, mwaka huu," alisema Mabula.

Waziri huyo alisema kunapokuwa na ramani za msingi inarahisisha pindi wanapotaka kupima kwa sababu huonyesha maumbile ya ardhi kama ni milima, mabonde au mito.

Mabula alisema awali walikuwa wakichukua ramani kwa kuzinunua kutoka Afrika Kusini au Kenya.

"Kwa sasa tutazizalisha wenyewe hapa hapa tayari tumeshawezeshwa. Tutakwenda kuimarisha mikoa yote na kuweka zile alama kwa ajili ya upimaji. Tutapunguza ule umbali wa kupima kwa wakati mmoja, utakuwa ni umbali mfupi mfupi na kasi ya kupima itakuwa inaongezeka," alisema Mabula.

Waziri huyo alisema malengo ya wizara ni kuhakikisha ardhi yote imepimwa kwa asilimia 100.

Mkuu wa Mkoa huo, Anthony Mtaka, alisema wilaya ya Makete inawezekana kupimwa yote kama watumishi wa ardhi na viongozi watakuwa tayari kiutendaji.

"Makete hivi karibuni itaondokana na migogoro ya ardhi kwa sababu ya kuongezeka kwa kasi ya upimaji ardhi na upimaji wa afya ya udongo ambayo itawasaidia wananchi kuongeza uzalishaji mazao ya kilimo,"alisema Mtaka.

Mbunge wa Makete, Festo Sanga, alimwomba waziri kutatua mgogoro wa mipaka na kubainishwa kwa maeneo kati ya Wilaya ya Makete na Mbarali, kwa kuwa wananchi wa Mbarali wanaendelea kuingia Makete.




Wanafunzi wa Shule ya Msingi Mtakuja ya Bagamoyo, mkoani Pwani, wakiwa wameshika viatu walivyopewa na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), kwa ufadhili wa kampuni ya Nissan, shuleni hapo jana. Wengine ni viongozi kutoka kampuni hiyo, TEA na Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Shule yaomba kujengewa uzio kukabiliana na wanyama

**Na Joseph Mwendapole**

SHULE ya Msingi Mtakuja iliyoko Kata ya Fukayosi, Bagamoyo mkoani Pwani, imewaomba wadau mbalimbali kuwasaidia ujenzi wa uzio shuleni hapo ili kukabiliana na wanyama wavamizi ambao wamekuwa wakisababisha uharibifu wa mali na mazao.

Ombi hilo lilitolewa jana na Mkuu wa Shule hiyo, Paschal Kitando, wakati akizungumza kwenye hafla ya kupokea viatu vilivyotolewa na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) kwa kushirikiana na Kampuni ya NISSAN.

Shule zilizopewa viatu ni Mtakuja, Visangalambwe, Konje na Mandamazingira na kila moja imepatiwa jozi 50 kwa ajili ya wanafunzi wanaotoka kwenye familia za wasiojiweza ambao wamekuwa wakihudhuria masomo wakiwa pekupeku.

Alisema shule hiyo imekuwa na kawaida ya kulima mboga na mazao mbalimbali kwa ajili ya matumizi ya chakula kwa wanafunzi, lakini yamekuwa yakivamiwa na kuliwa na mifugo.

"Tumeanzisha shamba kwa kushirikiana na wananchi na kulima mbogamboga kama jitihada za kuwapatia wanafunzi wetu lishe, lakini kikwazo ni wanyama wanaoingia na kula shambani kwa hiyo uzio utasaidia kuondoa changamoto hiyo," alisema.

Mwalimu huyo aliwaomba wadau mbalimbali wachangie ujenzi wa nyumba za walimu ili waweze kuwa karibu na kituo chao cha kazi kutokana kuwa mbali kutoka makao makuu ya halmashauri.

Alisema shule hiyo yenye wanafunzi 560 ina nyumba mbili za walimu wakati mahitaji halisi ni nyumba 12 huku idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa ikiendelea kuongezeka.

Meneja Rasilimali Watu wa TEA, Alice Lukindo, alisema mamlaka hiyo itaendelea kutafuta rasilimali kwa ajili ya kuendeleza elimu ili kusaidia sekta ya elimu.

Alisema lengo ni kuwawezesha wanafunzi kutimiza malengo yao kwenye elimu na kwamba imekuwa ikipata wafadhili mbalimbali ambao wamekuwa wakisaidia kwenye nyanja mbalimbali za elimu. "Ni matarajo yetu msaada huu utaleta hamasa kwenye masomo yao na pia, kuwaepusha na maradhi mbalimbali na tumeambiwa kwamba shule hizi zinafanya vizuri sana kitaaluma kwa hiyo, tunaomba muwe makini na masomo," alisema.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Bagamoyo, Delvin Maleko, aliwataka wazazi kuchanga kwa ajili ya chakula cha watoto wao.

"Katika shule zote za Bagamoyo ni shule yenu tu ambayo watoto hawapati chakula shuleni, maji yapo limeni mbogamboga watoto wale shuleni na kwa ufaulu walionao ina maana watafanya vizuri sana kwenye mitihani ya kitaifa," alisema.

"Hata watoto walipoimba hapa mbele waliomba chakula, kwa hiyo ni hitaji la msingi sana kwao na nyumba za walimu ni tatizo lakini tukishirikiana na serikali na wadau mbalimbali tutafanikiwa kuzijenga," alisema

Alisema iwapo walimu watapatiwa makazi karibu na shule watachangia kwa kiasi kikubwa maendeleo ya taaluma shuleni hapo kwa sababu kwa sasa wanalazimika kutumia muda mrefu kufika shuleni.

"Wekezeni kwa watoto wenu kwa sababu hawa ndiyo watarudi kuwasaidia kuendeleza miji yenu. Wako wahandisi hapa, walimu, mameneja na wakurugenzi wa kampuni mbalimbali ambao watatoka miongoni mwa hawa wanafunzi," alisema.

## Ujenzi shule mchepuo wa sayansi wakamilika

**Na Pilly Kigome**

UJENZI wa Shule ya Sekondari ya Mchepuo wa Sayansi kwa Wasichana ya mkoa wa Dar es Salaam, umekamilika kwa asilimia 90.

Ujenzi huo ni agizo alilolitoa Rais Samia Suluhu Hassan la kujengwa shule za maalumu za wasichana kwà mchepuo huo kwa kila mkoa.

Ofisa Elimu Sekondari Manispaa ya Ubungo, Mwalimu Voster Mjina, alipokuwa akizungumza na Nipashe ofisini kwake kuhusu maendeleo ya ujenzi wa shule hiyo.

Mjina alisema shule hiyo imekamilika kwa asilimia 90 na inatarijiwa kufunguliwa kesho kwa wanafunzi wa kidato cha tano pekee kwa awamu ya kwanza ya ujenzi. Alisema awamu ya pili ya ujenzi ukikamilika utapokea wanafunzi kuanzia kidato cha kwanza. Alibainisha kuwa tayari wanafunzi wameshadahiliwa na jumla ya wanafunzi 207 wanatarajiwa kuripoti shuleni kwa kuanza na masomo.

Mjina alibainisha shule hiyo iko mtaa wa Njeteni kata ya Kwembe, Manispaa ya Ubungo na ujenzi wake umegharimu Sh. bilioni tatu kwa awamu ya kwanza na awamu ya pili utàgharimu Sh. bilioni 1.1 na kwamba hadi kukamilika utagharimu Sh. billion 4.1.

Kwa mujibu wa Mjina, awamu ya kwanza ya ujenzi ilijumuisha ujenzi wa miundombinu yakiwamo madarasa 10, mabweni matano, nyumba tatu za walimu, maabara, bwalo la chakula na vyoo vya wanafunzi.

Awamu ya pili inayotarajiwa kuanza hivi karibuni, alisema itahusisha ujenzi wa mabweni manne, madarasa 10, jengo la teknolojia ya Habari na mawasiliano (TEHAMA), maktaba na nyumba za walimu, na unatarajiwa kukamilika Novemba, mwaka huu.

Alisema Shule hiyo imekwisha sajiliwa kwa jina la Shule ya Sekondari ya Wasichana Dar es Salaam . Pia alisema shule hiyo ya kisasa imesheheni vifaa na vitendea kazi vya kisasa yakiwemo majiko ya gesi, Vitabu vya kiada na ziada na chakula cha kutosha kwa ajili ya wanafunzi.

Kuhusu ajira, alisema tayari walimu 12 wamekwishiaripoti na kwa kuanzia watafundisha tahasusi za sayansi pekee zikiwamo Fizikia, Kemia na Hisabati (PCM), Fizikia, kemia na Baiolojia (PCB), Kemia, Baiolojia na Jiografia (CBG) na Kemia, Baiolojia na Masuala ya Lishe (CBN).

# Serikali yamaliza mgogoro kati ya kanisa na wananchi

**Na Munir Shemweta,**
NJOMBE

SERIKALI imehitimisha rasmi mgogoro wa muda mrefu baina ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Kusini, Njombe na wananchi wa kijiji cha Magoda na mtaa wa Lunyanywi, wilayani Njombe.

Uamuzi huo unatokana na maridhiano yaliyofikiwa baina ya pande zote za mgogoro baada ya timu iliyoundwa na kuhusisha wawakilishi kutoka kwa wadai na wale wa KKKT kuwasilisha ripoti yake. Timu hiyo ya wataalamu pia ilhusisha wataalam wa ofisi ya ardhi mkoa wa Njombe, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), polisi na ofisi ya usalama mkoa.

Akihitimisha mgogoro huo juzi mkoani hapa, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, alisema wananchi wanaodai wanatakiwa kupokea viwanja 400 kama kifuta jasho pamoja na urasimishaji wa makazi kwa wale walioingia kwenye eneo lenye mgogoro bila kufuata taratibu. Waziri pia aliitaka KKKT Dayosisis ya Kusini kulinda maeneo yake na kubainisha kuwa hakuna wa kuwalindia maeneo ya itakapotekea maeneo ya kanisa kuvamiwa, suala hilo lipelekwe katika vyombo vya sheria na si wizara.

Awali, wananchi wa kijiji cha Magoda na mtaa wa Lunyanywi walimweleza waziri kilio chao cha muda mrefu kuhusu mgogoro huo uliodumu kwa takriban miaka 22 bila kupatiwa ufumbuzi.

Walisema kuwa mgogoro huo una sura mbili na kuzitaja kuwa ni maeneo waliyodai kumiliki ndani ya skimu na maeneo ambayo wakati KKKT inapima ili kupata hati, lilivuka na kuingia kwenye maeneo ya watu binafsi.

Wananchi hao walitaka kuatambuliwa kama wamiliki wa maeneo hayo na si wavamizi na kuomba kulipwa fidia kwa mujibu wa sheria.

Utatuzi wa mgogoro baina ya KKKT na wananchi hao umekuwa ukiendelea kufanyika katika ngazi mbalimbali chini ya usimamizi wa Mkuu wa Mkoa wa Njombe na kufikia uamuzi kuwa KKKT itoe viwanja vya kifuta jasho kwa walalamikaji ili kuumaliza pamoja na kumega eneo la chuo lililojengwa nyumba na walalamikaji ili waendelezaji wabaki na maeneo waliyojenga




Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Aldof Mkenda na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Balozi Pindi Chana (waliokaa), wakishuhudia Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), Aneth Komba (kulia) na Mratibu wa Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Afrika, Boniface Kadili, wakibadilishana hati za makubaliano kuanza kusambaza vitabu vya masomo ya ukombozi mashuleni, baada ya kutiliana saini mkataba, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Vijana wengi hawana elimu kujikinga VVU

**Na Halfani Chusi**

UKOSEFU wa elimu sahihi kwa vijana jinsi ya kujikinga na maambukizi mapya ya Virusi vya Ukimwi (VVU), umetajwa ndio sababu ya vijana wengi kupata maambukizi hayo.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi mtendaji wa Baraza la Taifa la Watu Wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (NACOPHA), Deogratius Rutatwa, wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Sambamba na kauli hiyo Rutatwa aliwaalika wadau kushiriki mdahalo wa kitaifa wa kujenga ubia kati ya wadau na jamii, kuweka mkakati endelevu kupambana na maambukizi hayo kufikia malengo ya kitaifa na kimataifa ya vifo 0.3 ifikapo 2030.

Alisema vijana wengi wanapata maambukizi hayo kwa kutokujua njia za kujikinga pamoja na kutotumia kinga (kondomu) wakati wa tendo la kujamiiana.

"Serikali Kupitia Waziri wa Afya Ummy Mwalimu ilisema maendeleo ya watu wanaoishi na maambukizi hayo huku wanajua imefikia asilimia 96, walioko kwenye matibabu asilimia 98, waliofubaza asilimia 97, haya ni matokeo makubwa ambayo watanzania tunapaswa kuyalinda.

"Kazi hii sio ndogo, inahitaji juhudi za kimkakati wa pamoja kati ya NACOPHA, Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania TACAIDS, na Ofisi ya Waziri Mkuu tumekubaliana kutengeneza mkakati wa kitaifa utakao tokana na mjadala wa kitaifa ambao kilele chake utakuwa septemba." alisema Rutatwa.

Alisema wataweka mkakati kuonyesha Tanzania imelenga kutokomeza janga hilo na kuendelea kuunga mkono juhudi za serikali katika mapambano hayo, huku akiyataka mashirika mbalimbali kuendelea kuwaunga mkono ili kufanikisha mpango huo.

Ofisa Uraghbishi TACAIDS, Jumanne Issango alilipongeza baraza hilo kwa kuisaidia serikali kupambana na gonjwa hilo, akiwataka wadau mbalimbali kujitokeza kwa wingi kwenye mjadala huo kupata maoni ya pamoja ili kusukuma juhudi hizo.

## Tanzania, FAO zaungana kuboresha sekta ya uvuvi

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

SERIKALI kwa kushirikiana na Shirika la Chakula Duniani (FAO) inafanya marejeo ya sera na sheria za sekta ya uvuvi kwa lengo la kuiboresha kwa kuanzisha mamlaka itakayosimamia shughuli zote za uvuvi.

Kaimu Mkurugenzi wa Uvuvi kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Stephen Lukanga, aliyasema hayo katika warsha ya kitaifa ya kurejea na kupitia Sera ya Taifa ya Uvuvi ya mwaka 2015 na Sheria ya Uvuvi ya Mwaka 2003.

Lukanga alisema katika marejeo hayo wataangalia maeneo ambayo yanakosekana kwenye sera zilizopo hivi sasa ambazo zitafanyiwa marekebisho na kuanzishwa sera zingine.

Alisema kutafanyika marekebisho ya sheria ambayo itaendana na mazingira ya kumnyanyua mwananchi katika shughuli zote za uvuvi ikiwamo mvuvi.

Alisema wafanyabiashara wa samaki pamoja na mazao yake kulingana na kukua kwa sera zilizopo zinazokubalika kitaifa na kimataifa.

Lukanga alisema kuwa njia ya pekee ambayo inaweza kusimamia vyema sekta hiyo, ni kuanzisha mamlaka itakayosimamia maeneo yote ya shughuli za uvuvi kama zinazosimamia rasilimali za wanyamapori na misitu.

"Mabadiliko ya sayansi na teknolojia pamoja mabadiliko katika misingi ya usimamizi wa shughuli za uvuvi duniani ndiyo yanaleta msukumo wa kufanyika kwa marejeo ya sera na sheria zilizopo kwa sasa.

"Kwa hiyo na sisi tunaamini tunaweza kupiga hatua kwa kuanzisha Jeshi USU katika sekta ya uvuvi," alisema Lukanga.

Mratibu Dawati la Miradi kutoka Idara ya Uvuvi, Flora Luhanga, alisema sera itayopitishwa itaangalia haki ya kuishi, kulindwa kwa samaki, usalama wao pamoja na mlaji.

Pia alisema kutekeleza sheria zitakazodhibiti uvuvi haramu kwa kutokomeza zana za uvuvi ambazo hazijaruhusiwa, zinazoharibu mazingira ya samaki na mazalia yake.

Alisema sekta ya uvuvi imekuwa ikikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo kuvuliwa kwa samaki ambao hawajakomaa kupitia nyavu ambazo hazijaruhusiwa kisheria, matumizi ya kemikali na milipuko.

Alisema hali hiyo imekuwa ikishusha kiwango cha kuzaliana kwa samaki na kuchangia kuzorotesha soko la nchi za nje ambalo limekuwa likichangia asilimia 1.8 katika pato la taifa.

Luhanga alisema wamekuwa wakishirikiana na FAO katika nyanja mbalimbali za sekta ya uvuvi, ikiwamo uwezeshaji wa mafunzo mbalimbali ya kuendeleza sera za shughuli za uvuvi maeneo tofauti nchini.



# Wizara yazindua kituo cha huduma

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WIZARA ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, imezindua kituo cha huduma kwa wateja kitakachotumika kutoa huduma mbalimbali ikiwemo ya kuasili watoto kwa wenye uhitaji.

Kituo hicho kitasaidia kuondokana na tatizo la wizi wa watoto katika maeneo mbalimbali nchini.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Dk. Dorothy Gwajima, alisema hayo jana jijini hapa wakati wa uzinduzi wa kituo hicho na kubainisha kuwa kitakuwa na jukumu la kutoa utaratibu wa kuasili watoto na malezi ya kambo.

"Huduma hii itawezesha watu ambao wamekuwa na uhitaji la kuasili watoto kupata huduma hiyo ili kuondoa tatizo ambalo lilikuwa likijitokeza la wizi wa watoto, kwanini mtu aibe mtoto na watoto wapo wengi kwenye vituo vyetu wapige simu kwenye kituo hicho ili wapatiwe utaratibu wa kuasili watoto," alisema.

Dk. Gwajima alisema huduma nyingine itakayotolewa katika kituo hicho ni elimu kuhusu fursa mbalimbali za kiuchumi na mikopo yenye masharti nafuu kwa wanawake na makundi maalumu wakiwamo machinga, bodaboda, mamalishe na babalishe kupitia taasisi za fedha na serikalini.

"Kituo pia kitatoa mwongozo na utaratibu dhidi ya manusura wa ukatili na unyanyasaji wa kijinsia na kwa watoto. Msaada wa kisheria kwa manusura wa ukatili wa kijinsia na kwa watoto na haki za wanawake na wajane, utaratibu kwa wahanga wa usafirishaji haramu wa binadamu," alisisitiza Dk. Gwajima

Alisema jukumu jingine la kituo hicho ni kusimamia utaratibu wa kuokoa watoto wanaoishi mazingira hatarishi na kufanya kazi mitaani na wazee wasiojiweza na familia duni.

Pia alisema kituo kitashughulikia ukatili kwa watoto mitandaoni, malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto, ushauri kwa vijana balehe, msaada wa kisaikolojia katika jamii,miongozo kuhusu utatuzi wa migogoro ya familia na ndoa, marekebisho ya tabia na elimu kwa watoto.

Utaratibu wa kusajili na kulipia huduma mbalimbali zikiwemo za mitihani, usajili wa makao ya watoto, vituo vya kulelea watoto mchana (day care centres) na Asasi zisizo za kiserikali.

"Kituo pia kitoa utaratibu wa kusajili wa asasi zisizo za kiserikali (NGO), ulipaji wa ada mbalimbali na uwasilishaji wa taarifa za robo na za mwaka. Huduma zingine ni usajili wa kujiunga na vyuo vya maendeleo ya jamii na ustawi wa jamii, malipo ya ada na upatikanaji wa matokeo ya mitihani"alisema

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. John Jingu, alisema kuanzishwa kwa kituo hicho kutamuondolea mteja usumbufu usio wa lazima wa kusafiri mwendo mrefu na kuingia gharama zisizo za lazima kwenda kupata huduma wizarani ambazo angepata huko aliko.

"Na badala yake akipata changamoto zinazohitaji wizara iingilie kati basi ataweza kupewa ushauri, mwongozo na ikibidi huduma akiwa katika maeneo ya makazi yake akiendelea na shughuli zake za maendeleo,"alisema Dk. Jingu

Alisema mpango wa muda mrefu ni kupanua wigo wa utoaji wa huduma hizo za mawasiliano na jamii kutoka matumizi ya simu pekee na kufikia kutumia njia nyingi zaidi za mawasiliano kama vile barua pepe, ujumbe mfupi na mitandao ya kijamii ili wizara isogee karibu na jamii.

# DAWASA yataja vipaumbele kumaliza uhaba wa maji Dar

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar as Salaam (DAWASA), imetaja vipaumbele vyake kwa mwaka 2023/24 vya kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji safi ikiwamo utekelezaji wa miradi ya kimkakati saba itakayogharimu Sh. bilioni 425.9.

Miradi hiyo ni pamoja na bwawa la Kidunda, ujenzi wa mtambo wa kuzalisha maji wa Rufiji, Kwala, Pangani Kibaha, Kimbiji-Kigamboni hadi jirani na Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA), Kusini mwa Jiji la Dar es salaam na uchimbaji visima virefu tisa eneo la Kigamboni.

Akizungumza jana na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa miradi na mwelekeo wa mwaka huo, Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Kiula Kingu, alisema miradi hiyo inalenga kuongeza wingi wa maji yanayozalishwa, kuongeza uwezo wa kuhifadhi maji.

Pia alisema kuimarisha mfumo wa usambazaji maji na kuimarisha huduma katika maeneo ambayo hayana mtandao hasa yale ya pembezoni.

Kadhalika, alisema DAWASA imejipanga kikamilifu na kuchukua hatua za makusudi za kuboresha usafi wa mazingira kupitia miradi mikubwa na midogo.

"Hii ni kwasababu upatikanaji wa maji unapoongezeka unapaswa uambatane na usimamizi madhubuti wa usafi wa mazingira," alisema.

Katika wilaya za Kinondoni na Ilala, miradi ya kuchakata majitaka itajengwa maeneo ya Mbezi Beach na Buguruni.

"Mradi wa Mbezi Beach unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya serikali na Benki ya Dunia na Sh. bilioni 132.3 zitatumika kujenga mtambo wa kisasa wenye uwezo wa kuchakata lita milioni 16 kwa siku," alisema.

Kingu alitaja miradi mingine ni wa kujenga mfumo wa kukusanya majitaka na maeneo nufaika katika awamu hiyo ni Mbezi Beach, Kilongamwima, baadhi ya maeneo ya Kawe na Salasala na utekelezaji umeanza na kwamba makandarasi wanaendelea na maandalizi ya ujenzi.

Hata hivyo, alisema DAWASA imekuja na ubunifu wa kujenga mifumo na mitambo midogomidogo ya kuchakata majitaka inayojengwa maeneo ya pembezoni ambapo zaidi ya lita 780,000 za majitaka zitakuwa zikichakatwa kwa siku.

Alisema miradi hiyo ambayo pia itajumuisha ujenzi wa vyoo vya umma 30, itasaidia kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma hizi muhimu na hivyo kuboresha usafi wa mazingira.

"Miradi hii itasaidia wananchi kupata huduma za usafi wa mazingira kwa gharama nafuu karibu na maeneo wanayoishi, wakandarasi wanaotekeleza miradi wanaendelea na ujenzi," alisema.

Alisema gharama za miradi hiyo ni sh.bilioni 25.7 na wanufaika wa miradi hiyo wanakadiriwa kufikia milioni 1.8.

"Miradi hii ni ya kisasa na katika mfumo wake wa uchakataji majitaka itatoa gesi asilia kwa ajili ya kupikia, itatoa mbolea itakayoweza kutumika katika kustawisha bustani za miti na majani lakini pia maji yatakayochakatwa yataweza kutumika kwa ajili ya shughuli za umwagiliaji, usafishaji wa barabara na mitaro au kupoozea mitambo," alisema.




Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye ulemavu, Prof. Jamal Katundu akizungumza wakati wa kufungua kongamano la maadhimisho ya Siku ya Vijana Kimataifa jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Chatanda: Wananchi changamkieni fursa

**Na Thobias Mwanakatwe,** MANYONI

MWENYEKITI wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) Taifa, Mary Chatanda, amewataka wananchi kuchangamkia fursa za ajira zinazopatikana kwenye miradi mbalimbali inayotekelezwa na serikali katika maeneo yao ili wajikwamue kiuchumi.

Akikagua utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) wilayani hapa, Chatanda alisema ili kupunguza tatizo la upatikanaji wa ajira, ni muhimu kwa wananchi kufanya kazi kwenye miradi hiyo kupitia ajira za muda zinazopatikana hali itakayowafanya kuongeza kipato.

Pia alisema wananchi wahakikishe wanajitolea nguvu kazi kwenye miradi mbalimbali inayotekelezwa na ili kuunga mkono juhudi za serikali za kupeleka huduma kwa wananchi.

Alisema wananchi wakijitolea nguvu kazi itasaidia miradi hiyo kukamilika kwa wakati na kupunguza gharama za miradi hiyo kufuatia kuwepo kwa nguvu za wananchi.

Hata hivyo, Chatanda alizitaka familia kuwapeleka watoto wao shule kupata elimu na sio kuwafanyisha kazi ambazo zinasababisha watoto hao kutokwenda shule.

Alisema kuna baadhi ya familia watoto hawaendi shule kwasababu ya kazi za kuchunga mifugo na wakati mwingine kazi za shamba, hali inayosababisha watoto hao kukosa haki zao za msingi za kupata elimu.

Naye Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Singida, Martha Mlata, aliishukuru serikali kwa kuendelea kutatua kero za wananchi kwa kutekeleza miradi inayotoa huduma stahiki kwa jamii.





# Othman aelezea imani maridhiano

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema kuanza kwa vikao vya Kamati ya pamoja ya Maridhiano ya Kisiasa kati ya Chama cha ACT -Wazalendo na Chama Cha Mapinduzi (CCM), ni hatua muhimu ya kutia moyo na ya kuleta matumaini ya kuwapo na kuendelea mjadala wa masuala yanayohusu mustakabali mwema wa Zanzibar .

Othman aliyasema juzi hayo nyumbani kwake, Chukwani, nje kidogo ya mji wa Zanzibar, alipokutana na Balozi Mdogo wa Uingereza nchini Tanzania, Rick Shearn, aliyetaka kujua pamoja na mambo mengine ya maendeleo ya kamati hiyo ya pamoja iliyoundwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Alisema hivi sasa kamati hiyo imeanza vikao vyake kwa kujadili maeneo na ajenda muhimu na mahususi na namna ya utaratibu bora utakaotumika katika kuyajadili masuala muhimu ili kufikia mwafaka kwa malengo yaliyokusudiwa ya mustakabali wa Zanzibar na watu wake.

Aidha, alisema anaamini katika vikao hivyo vya awali maeneo yote muhimu yanayohitaji kufanyiwa mabadiliko na mageuzi makubwa yameainishwa kwa kuwasilishwa na kujadiliwa kwa pamoja katika kutafuta maslahi bora ya Zanzibar na watu wake.

Makamu huyo alisema kuwapo kwa hatua hiyo ni fursa muhimu kwa Zanzibar katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi wa 2025 katika kufanya mabadiliko na mageuzi yanayotarajiwa na wananchi wa Zanzibar katika kuweka matumani ya mustakabali wa nchi yao. Alisema majadiliano hayo ya awali yamegusa katika maeneo muhimu yote likiwemo suala la mageuzi na mabadiliko katika masuala ya uchaguzi ikiwemo tume inayosimamia uchaguzi ili kuifanya kuwa taasisi imara kwa maendeleo na mustakabali mwema wa Zanzibar.

Pia alisema ajenda ya masuala ya uchaguzi inaendelea kama jambo muhimu katika misingi ya mjadala huo kwa kuwa unalenga maisha ya Wazanzibar, biashara kwa Zanzibar pia uwekezaji kwa maendeleo ya nchi.

Alisema Zanzibar inahitaji uwekezaji na wawekezaji wanahitaji kuwekeza fedha zao katika eneo salama na lenye utulivu ili waweze kufanya biashara na wageni kutembea Zanzibar kupitia sekta ya utalii.

Aidha, alisema masuala mengi yanayogusa mambo muhimu yakiwamo mabadiliko katika sekta za umma na kuwapo uwajibikaji na utawala wa sheria yameainishwa kwa kuwa ni mambo yatakayosaidia kuondosha udhaifu katika maeneo mbalimbali ili kujenga maendeleo endelevu ya Zanzibar.

Akizungumzia suala la Katiba Mpya , Othman alisema hilo ni suala la Muungano lakini linagusa maendeleo ya masuala kadhaa ya Zanzibar moja kwa moja na kwamba kuna masuala mengi yanayohitaji kufanyiwa mageuzi katika usimamizi na uendeshaji wake ikiwemo suala la haki jinai na uchaguzi wa wabunge na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Naye Balozi Shearn alitaka kufahamu iwapo suala la Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pia linaweza kuathiri mustakabali wa Zanzibar katika uchaguzi ujao wa 2025 na utekelezaji wa masuala mbalimbali ikiwamo uchaguzi wa Zanzibar.

# Ujio msanii China kupaisha utalii Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema ujio wa nyota maarufu wa filamu kutoka China, Jin Dong, utaendelea kuifungulia Zanzibar soko la utalii China.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo Ikulu, Zanzibar alipotembelewa na msanii huyo maarufu China ambaye yuko Zanzibar kwa ajili ya kutengeneza filamu.

Alisema ujio wake ni fursa adhimu kwa Zanzibar kutangazwa kimataifa hasa kupitia sekta ya utalii ambayo ni sekta mama ya uchumi wa taifa.

Rais Mwinyi alisema Zanzibar ina vivutio vingi vya utalii, ukiwamo utalii wa fukwe safi nyeupe zinazovutia watu wengi duniani, utalii wa utamaduni, utalii wa mji mkongwe, utalii wa michezo, utalii wa visiwa na wa mikutano.

Naye nyota huyo, Jin Dong, alielezea furaha yake ya kufika Afrika kwa mara ya kwanza tena ndani ya visiwa vya Zanzibar kwa nchi za Afrika Mashariki.

Alisema mbali na safari ya sanaa pia ujio wake unaimarisha uhusiano wa undugu na urafiki uliopo baina ya China na Tanzania, ikiwamo Zanzibar.

Dong aliahidi kuwa balozi mzuri wa kuitangaza Zanzibar kwa utalii na alieleza imani yake ya kuwavutia wachina wengi kuja kutalii visiwa vya Zanzibar.

Miongoni mwa maeneo ya utalii aliyotembezwa msanii huyo ni kisiwa cha Mnemba, Mji Mkongwe maeneo ya Forodhani na Ngome Kongwe.

Dong ni nyota mkubwa China mwenye wafuasi wa mitandao ya kijamii zaidi ya milioni 15. Mbali na kazi za sanaa pia ni Mwanasiasa na Naibu Mkurugenzi wa kikundi cha Sanaa cha Serikali cha Utamaduni.



Meneja Masoko wa PepsiCo kwa Vinywaji Afrika Magharibi, Mashariki na Kati, Karen Veysey (kushoto), Kiongozi wa Biashara ya Vinywaji wa kampuni hiyo kwa Afrika Magharibi, Mashariki na Kati, Isabel Coetzer (wa pili kushoto), Mkurugenzi wa Leostar International Ltd, Sanjay Mehta na Meneja Biashara wa Leostar International Ltd, Boikgantsho Kgwadi (kulia), wakishuhudia uzinduzi rasmi wa vinywaji vya Ceres Nectar vilivyofanyiwa maboresho, jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Waziri asisitiza wanawake, vijana kujikita kilimo, uzalishaji chakula

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Muhagama, amesema sekta ya kilimo kwa sasa imeajiri takribani asilimia 40 na wananchi wa Zanzibar.

Pia amesema inakadiriwa kuwa zaidi ya asilimia 70 ya wananchi wanategemea sekta hiyo katika kujikimu kimaisha.

Akizungumza juzi wakati hafla ya ufungaji wa maonyesho ya Siku ya Wakulima (Nanenane), Dole Kizimbani, Zanzibar, alisema serikali imeongeza bajeti kwa wizara inayoshughulikia kilimo katika mwaka wa fedha 2023/24 ambayo imeidhinishwa kutumia Sh. bilioni 98.716 kulinganisha na Sh. bilioni 53.59 kwa mwaka 2022/23.

Serikali ya Zanzibar, alisema inaendelea kuweka mazingira wezeshi ya kukuza kilimo na kutekeleza mikakati ya kuleta mageuzi makubwa katika sekta hiyo kwa kuwekeza fedha zaidi.

Alisema hiyo inadhirihisha kuwa Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi ameridhia pia katika nia yake thabiti ya kuendeleza kilimo na kuamua wakulima kupatiwa ruzuku za pembejeo za kilimo kwa nafuu ya asilimia 50 ya gharama zake.

"Haya ni maamuzi ya kijasiri yenye nia na thabiti ya Rais Mwinyi kujali sekta ya kilimo na wakulima wa Zanzibar. Tunaamini kupitia wizara mtayasimamia vizuri na yataongeza tija kwenye ustawi wa kilimo nchini," alisema.

Waziri Mhagama alisema hiyo inathibitisha nia ya serikali kuhakikisha inafikia azma yake ya kujitosheleza kwa mahitaji ya chakula na azma hiyo inajionesha kwa vitendo.

Akizungumzia kaulimbiu ya maonyesho hayo 'Vijana, Wanawake ni Msingi imara wa Mfumo Endelevu ya Chakula', alisema inadhihirisha kuwa makundi hayo ndiyo msingi imara wa maendeleo ya chakula. Alisema kaulimbiu hiyo imetilia mkazo kutumia nguvu kazi ya vijana katika uzalishaji wa chakula nchini.

Mhagama alisema wanaamini mageuzi makubwa ya sekta ya kilimo katika kuongeza uzalishaji wenye tija, kukuza kipato cha wakulima na pato la taifa na uimarishaji wa afya ya jamii kwa Wazanzibari tegemeo kubwa ni vijana na wanawake.

Kwa mantiki hiyo, alisema mageuzi ya kilimo tegemeo kubwa ni vijana na wanawake, hivyo ni matumaini yake kuwa vijana na wanawake watatumia uchumi wa bluu na kijani ambao ndiyo utaifikisha nchi katika maendeleo endelevu.

Alisema Afrika ni bara lenye vijana wengi na kwamba asilimia 60 ya watu wake ni chini ya umri wa miaka 25 na vijana wapatao milioni 12 hutoa nguvu kazi yao katika kilimo kila mwaka.

"Tanzania ina ardhi nzuri na baadae mazao ya chakula yatageuka kuwa mazao ya biashara, hivyo tuendelee kufuata ushauri wa wataalamu, kuiunga mkono serikali hasa kwa juhudi hizi anazozifanya Rais Mwinyi katika kuwashirikisha vijana kwenye sekta hii ya kilimo," alisema.

Pia alisema alisema wanawake wana mchango mkubwa katika ujenzi wa taifa, hivyo ni vyema kulima na kuongeza mazao ya chakula na kuweka mifumo mizuri ya chakula na lishe kwa nchi na kuongeza mapato ya wanawake, vijana na serikali kwa ujumla.

Naye Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Shamata Shame Khamis, alisema wizara itaendelea kuyafanyia kazi maelekezo aliyoyatoa Rais Mwinyi ikiwamo kuwa na mazao ya mkakati kwa kila wilaya na kuendelea kuwahamasisha wananchi kuendelea kulima ili kuona Zanzibar haipati tishio la kukosa chakula.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Seif Shaaban, alisema maonyesho hayo ni ya tano ambayo yamepata mafanikio makubwa kwa washiriki kutumia fursa ya kukuza kilimo.

Alimpongeza Rais Mwinyi kwa kujitoa na kudhihirisha kivitendo dhamira yake ya kukuza kilimo Zanzibar kwa kuwa katika kuimarisha zao la mpunga kwa mwaka 2022/23, alitoa mbegu za mpunga tani 88 kwa wakulima zenye thamani ya Sh. milioni 227 ambazo zilisambazwa kwa Unguja na Pemba na kusaidia kupatikana kwa tani 1,000 za mbolea.



## WAMEFIKIA PABAYA

UKURASA 12



Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE



# MOLA MWEPUSHE

FAMILIA ya mwanamuziki mkongwe wa nyimbo zenye hisia kali ya mapenzi, Celine Dion, imesema hali ya kiafya ya msanii huyo bado ni ya wasiwasi na kwamba juhudi za kusaka tiba zinaendelea.

Hata hivyo, ndugu hao wamesema wana matumaini siku moja watapata tiba ya ugonjwa adimu ambao unamtesa staa huyo.

Dada wa msanii huyo maarufu duniani, Claudette, alielezea afya ya Celine kuwa bado ina mashaka kutokana na familia kushindwa kupata tiba ya ugonjwa unaomsumbua ndugu yao.

Katika mahojiano na Le Journal de Montreal, amefichua kwamba mpaka sasa Celine ameshindwa kupata dawa ya kudhibiti ugonjwa huo unaoshambulia mishipa ya mwili.

Ameeleza kwamba pamoja na mdogo wake kukabiliwa na mateso ya maumivu, bado wanaweka matumaini makubwa kuwa siku moja watapata tiba sahihi.

"Hatuwezi kupata dawa yoyote ambayo inafanya kazi, lakini kuwa na matumaini ni muhimu." Amesema.

Celine amepata mafanikio katika kazi yake ya muziki na nyimbo zake zimekuwa na kiwango cha juu cha kupendwa kwa miongo kadhaa.

Ameongeza kuwa dada yao Linda amehamia nyumbani kwa Céline ili kutoa msaada zaidi kwa wanawe watatu. Watoto hao René-Charles, Eddy na Nelson wanashirikiana na mama yao huyo mkubwa kumuuguza.

Amesema kazi ya utafutaji wa tiba inaendelea kwa kasi, ikiwa pamoja na kuwashirikisha watafiti wa tiba na madaktari bingwa.

Claudette amesisitiza kwamba bado ana wasiwasi kuhusu dada yake, lakini aliwahakikishia mashabiki wa Céline kwamba wanafanya juhudi kubwa kumponya.

"Ninafikiri kwa uaminifu kwamba anahitaji kupumzika zaidi. Yeye (Celine) anakuwa juu zaidi ya matumaini, yeye daima anajaribu kuwa bora." Ameongeza.

Kutokana na ugonjwa huo mwili wa Celine umekuwa dhaifu na kusababisha familia kupunguza majukumu yake kwa ajili ya kupata muda wa kupumzika.

Kati ya hatua zilizochukuliwa ni kusitisha matamasha ya burudani pamoja na kuhudhuria sherehe mbalimbali.

Kulingana na Kliniki ya Mayo, ugonjwa unaomkabili msanii huyo humfanya mtu kuwa katika hali ngumu na ni hali isiyo na tiba.

Ugonjwa huo hushambulia mishipa na kusababisha mshtuko wa misuli na kuidhoofisha. Matatizo hayo humuathiri mtu mmoja kwa kila watu milioni moja.







BASI SAWA

## Velma awavuruga mastaa



Mrembo anayekuja kwa kasi kwenye muziki, Velma Visembo, amekuwa kivutio kwa mashabiki wengi na kutabiriwa kuwapiku wasanii wakike wa nchini Kenya.

Akizungumza na BT meneja wa Visembo, Roy Captain amesema mwanamuziki huyo ambaye yuko chini ya lebo ya Super Squad Kenya, ameanza kukamata chati mbalimbali za muziki kupitia wimbo wake mpya 'Buta Ka'.

"Visembo ni tishio kwa mastaa wakike hapa Kenya, wanaona kama anataka kuchukua nafasi yao kutokana na uwezo, kipaji na urembo wa mwimbaji wangu, nawaomba wapenzi wa muziki hapo Tanzania pia waendelee kumsapoti ili afike mbali," amesema Roy Captain.

## Starshine amvizia Karen Simba

Msanii anayekuja kwa kasi kwenye Bongo Fleva, Starshine, ameweka wazi kuwa ngoma yake mpya, 'Mi Aliento', imetokana na mwigizaji mrembo Karen Simba.

Starshine, ameliambia gazeti hili kuwa Karen Simba ni zaidi ya rafiki kwake na wazo la kuandika wimbo huo alilipata kwenye mazungumzo na mrembo huyo anayefanya vizuri kwenye tamthilia mbalimbali.

"Mi Aliento ni neno analopaswa kuambiwa mtoto mzuri yeyote yule hasa Karen Simba ambaye ndio sababu ya mimi kufanya wimbo huu ambao utatoka muda wowote kutoka sasa, naamini wadada wazuri wote utawahusu," amesema Starshine.





# WAMEFIKIA PABAYA

UGOMVI kati ya Haromonize na Kajala sasa umefikia kilele kisichovumilika tena baada ya wawili hao kila mmoja kumuita mwenzie jina lisilofaa.

Kwa wiki kadhaa wawili hao wamekuwa katika mvutano mkali unaotokana na kitendo cha Harmonize kutoa wimbo mpya ambao unamuelezea Kajala kama mwanamke mwenye tamaa.

Katika kujibu mapigo Kajala alisema kamwe yeye hana tamaa na kila kitu ambacho Harmonize alikifanya ilitokana na mapenzi yao na wala hakumtuma.

Kajala alimfananisha Harmonize kama mtu aliyechanganyikiwa na hivyo yeye hawezi kubishana naye na kumtaka amuache afanye mambo yake.

Kitendo cha kufananishwa na kichaa, kimemchukiza Harmonize na kumfanya kuanza kutiririsha siri nyingi zilizojificha ikiwa na kueleza bayana kwamba hakumtongoza binti yake Paula, bali yeye ndiye alimtaka kimapenzi huku akijua anaishi na mama yake.



# Diamond, Harmonize uso kwa uso tena

PENGINE itatokea miujiza hivi karibuni na kuwaona wanamuziki wawili wa Bongo Fleva mahasimu nchini, Diamond Platnumz na Harmonize wanapanda jukwaani pamoja na kutoa burudani kabambe.

Miujiza hiyo inaweza kushuhudiwa kutokana na Harmonize kukubali kutumbuiza katika tamasha la wasafi litakalofanyika Mtwara hivi karibuni.

Harmonize ameandika katika ukurasa wake wa Instagram kuwa amekubali kutumbuiza tamasha hilo ambalo linaandaliwa na Wasafi na kuwahimiza mashabiki wa muziki kukata tiketi kwa wingi.

Diamond Platnumz alizungumza hivi karibu mbele ya vyombo vya habari kuwa Alikiba na Harmonize wanaweza kushiriki kwenye Wasafi Festival.

# UKIZIONA PICHA HIZI

**Na Adam Fungamwango**

Miaka ya 1980, hadi katikati ya miaka ya 1990, kabla ya televisheni kuenea majumbani kuanzia katikati ya miaka ya 1990, vijana na watoto wengi walikuwa wakienda maeneo mbalimbali ilikuona sinema.

Wengine walienda kwenye majumba makubwa ya sinema. Hao ni kwa wale wenye uwezo. Wengine walikwenda maeneo ambayo yalikuwa yanaafadhali kidogo. Lakini wengi wao hasa watoto walikuwa wakienda kwenye sehemu ambazo kwa sasa zinaitwa 'vibandaumiza'.

Huko utakuta mtu kazungushia tu magunia na ndani kaweka televisheni yake, akionyesha filamu mbalimbali.

Achilia mbali filamu za Kichina, ambazo nyingi ni za sanaa za mapigano, na kihindi ambazo tutakuja kuzizungumizia siku nyingine. Leo tutaziangalia filamu za kizungu.

Kulikuwa na filamu nyingi maarufu za kizungu ambazo hakuna kijana au motto ambaye alitaka kuzikosa. Leo tuna kwenda kuangalia filamu hizo.

**War Bus**

Ni filamu maarufu sana kwa Wabongo, ambayo ilitoka mwaka 1985. Mastaa wa picha hii ni Daniel Stephen, Romano Kristoff na UrsAlthaus.

Msingi wa picha hii ni vita ya Vietnam. Ni makomandoo watatu wa Kimarekani waliokwenda kuwaokoa mateka walioshikiliwa na 'wavete', kama walivyokuwawakiitwawatotowakatihuo.

Kilichovutiazaidiwatazamajiwengiwafilamuhiyo, siyoopereshenihiyo, balinistailiyamakomandoohaoambaowaliamuakutekabasiyashulenakulitumiakamausafiriwakwendakuwaokoleawatuwao. Ilestailiyaulinziwammojakukaambeleyaboneti la basi, mwinginejuukwaajiliyaulinzi, mwinginendani, pamojanambwembwezao, ndiyomsingiwapichahiikupendwa.

**American Ninja**

Hiipianifilamuambayoiliwanyimawatuusingizi, ikitoamwaka 1985 kama 'War Bus'.

Wakubwa, vijananawatotowaKibongowaliipendasanafilamuhii, ikimhusishastaammojaanaitwa Michael Dudikoff. HuyuniaskariwaKimarekaniambayepiaanaujuzimwinginewakupigananawatuwanaitwamaninja, ujuzialioupataakiwamdogo.

Humuanatwangananamaninjakisawasawanakuwshinda, kiasi cha kuwamojayafilamu bora sananakukumbukwahadileo.

**No reatreat, no surrender**

Filamuhiiilitokamwaka 1986. Hiisiyoyakivitakama 'War Bus'. Walasiyoyamapanganasanaazakininja. Pichahilini la sanaawamapigano. Humondanozimepigwabalaa. Stelingikwenyefilamuhuunistaaaliyekuwamaarufusanawakatihuo, Jean Claude van Damme. Huyualisifikasanakwamatekeambayondiyoyaliyokuwayanampazaidiushindi. Ni mojakatiyafilamumaarufunailiyopendwasana.

**KomandoKipensi**

Jinahalisiyapichahilini 'Deadly Pray'. Lakininadhanihadileosiwengiwanaojuajinahalisiyafilamuhii. Lakiniukiwaambia 'Komandokipensi', kilamtuatasemaanaifahamu.

Sidhanikamakunamtoto au kijanawamiakaya 1980 mpaka 2000, ambayehaifahamufilamuhii. Ilitokamwaka 1987.

Jamaaanaitwa Troy Donahue, au kwajina la pichani Mike Danton. Huyunijeshi la mtummoja. Anapiganaakiwaamevaapensitu, ndiyomaanawakamwitahivyo. Alimchokozawenyewe. Walikuwahawajuikuwanimwanajeshimstaafu. Walitakakumfanyachambo. Ikawani vita vyaajabu.

**Delta Force**

Ilitokamwaka 1986. Ni mojakatiyafilamumaarufusanakwaWabongowakatihuo. Staawafilamuhiinimkongwe Chuck Norris. Ni picha la kivita.



FILAMU

# Ndoa ya Kisirani: Ukilikoroga utalinywa la moto

**Na Adam Fungamwango**

WIMBI la watoto wa mitaani kwenye nchi yetu husababishwa zaidi na migogoro kwenye familia.

Baba na mama wakitengana mara nyingi wanaoathirika ni watoto kwa sababu wao wanawategemea wote wawili kwenye malezi bora na mahitaji muhimu.

Mke au mume wakitengana wenyewe huwa hawaathiriki kwa sababu kila mmoja anatengeneza maisha yake mengine.

Tatizo linakuwa kwa watoto ambao ni lazima sasa watalazimika kukaa sehemu moja katika wazazi hao na mara nyingi ndipo tatizo linapoanzia.

Sitaki kuingia kwa undani sana, ila tukiangalia filamu ya 'Ndoa ya Kisirani' ambayo inaakisi hiki kinachoainisha hapa.

Imechezwa na wasanii Arafa Said akiigiza kama Walivyo, Juma Mbwana, akacheza kama Mbwana, Fatuna Chole mama mdogo wa Walivyo, Said Abdallah, Mjomba wa Walivyo, Latifa, Shangazi wa Mbwana, Hussein Hassan, Mjomba wa Mbwana.

Ndoa ya Mbwana inaanza kuingia mushkeli kwa sababu ya maisha duni aliyonayo.



Mkewe kapata walimu, ambao ni wanawake wa mtaani wakimwambia ajiongeze kwani mumewe hawezi kumtekelezea mahitaji yote.

Anaingia kwenye mapenzi haramu na kijana mmoja anaitwa Omari.

Ndoa inakuwa tafrani kila siku ugomvi, huku mke akionyesha kabisa kuwa hahitaji kuishi na mume tena.

Akarudi nyumbani kwa mama yake mdogo na kumuongopea mambo mengi ili kutengeneza mazingira mwanaume aonekane hafai.

Hakuliki wala hakulaliki, Walivyo anaamua kufungasha kilicho chake na kwenda kukaa kwa mama yake mdogo.

Kutokana na kukosa uangalizi mzuri, Walivyo akila raha na mchepuko wake, ilisababisha mtoto kugongwa na gari, akafariki dunia.

Kwenye msiba kunazuka kizaazaa, Mbwana akimtuhumu mkwewe kuwa ndiye aliyesababisha yote kwa kumpokea mke wa mtu na kuishi naye.


Mama naye hajamuacha, akamshambulia kuanzia unywele hadi kucha, ikawa ni mshikemshike tu msibani hapo.

Hata mazishi yenyewe yalifanyika kwa tabu na mgogoro mkubwa.

Ulipoisha wakakaa na kuzungumza kila mmoja akitoa malalamiko yake.

Mwisho wa siku ilikuja kuonekana kuwa kweli Walivyo na mama yake mdogo wana makosa na si Mbwana.

Pamoja na kuomba amrudie mkewe, lakini Mbwana anashikilia msimamo wa kumpa talaka mkewe na kubaki na mtoto wake mmoja wa kike aliyebaki.



# Rapa Lanez aanza kutumikia kifungo

RAPA kutoka Canada, Tory Lanez ameanza kifungo cha miaka 10 jela baada ya kupatikana na hatia ya kumpiga risasi na kumjeruhi aliyekuwa mpenzi wake, nyota wa hip hop Megan Thee Stallion.

Alimpiga risasi Megan miguuni wakati wa mabishano baada ya tafrija ya kuogelea kwenye nyumba ya Kylie Jenner mnamo 2020.

Licha ya kupewa hukumu hiyo, Lanez alisema kuwa bado anamjali Megan kama mtu wake muhimu.



## Yul aapa kusema yote

MWIGIZAJI mwenye utata Yul Edochie, ameapa siku moja atafichua ukweli kuhusu ndoa yake ya pili baada ya baba yake Pete Edochie, kusema kuwa hakuwa na habari nayo.

Kupitia ukurasa wake wa Facebook, mwigizaji huyo alichapisha kipande cha picha ya Judy ambaye ni mjamzito akiwa na baba yake kwenye filamu wakitabasamu.

Mzee Edochie wakati akihojiwa na mwanahabari Chude Jideownwo, alibainisha kuwa hakufahamu kuwa Yul alikuwa ameoa mke wa pili kwasababu yeye hajihusishi na mambo ya mtoto wake.


## Ne-Yo haombi radhi

MWIMBAJI na mtunzi wa nyimbo kutoka Marekani, Ne-yo amesisitiza hataomba radhi kwa hatua yake ya kuwakemea wazazi wanaowaruhusu watoto wao kubadili jinsia.

Licha ya kukabiliwa na anguko la kifedha kutokana na maoni yake hayo, Ne-Yo amezidi kuwalaumu wazazi hao kwamba si maadili kuwaacha watoto kubadilisha maumbile ambayo Mungu amewaumba.

"Kwanza kabisa, sitaomba radhi kwa kuwa na maoni juu ya jambo hili. Mimi ni mwanamume mwenye umri wa miaka 43, ninalea wavulana watano na wasichana wawili, sawa? Huo ndio ukweli wangu," ameandika





## Kuna jambo miwani ya Simi

MWANAMUZIKI nyota wa Nigeria, Simi ameeleza jinsi alivyokuwa na hisia tofauti mbaya miaka mitatu baada ya kumzaa binti yake Adejare.

Katika video hiyo iliyotumwa kwenye akaunti yake ya Tiktok, alisimulia kile alichokiita 'hadithi ya kwikwi' kwa watazamaji wake, akibainisha kuwa sasa lazima avae miwani.

Alieleza tangu ajifungue binti yake ambaye sasa ana umri wa miaka mitatu amekuwa na uoni hafifu kiasi ambacho madaktari wamemshauri kutumia miwani kwa ajili ya kumsaidia.

## Skales bora umejitambua

MWANAMUZIKI wa Nigeria, Skales amesema kuna wakati alizichapa na msanii mwenzake Kizz Daniel baada ya kuzidiwa na kilevi.

Mwimbaji huyo ambaye jina lake halisi Raoul John Njeng-Njeng, amefichua hayo wakati wa mahojiano yake na redio moja na kueleza yeye na Kizz Daniel walipigana katika makazi ya Timaya na hilo lilikuwa kosa lake.

"Nimetengeneza mahusiano ya dhati na watu wa tasnia hii. Nimekuwa na mabifu kadhaa, zingine ninazozifahamu na zingine nisizozijua. Lakini ugomvi wangu na Kizz Daniel lilikuwa kosa langu." amesema



HABARI KASKAZINI

## Adaiwa kuuawa akilinda mazao

**Na Mary Mosha**, SIHA

MKAZI wa Kijiji cha Ngaroni, Kata ya Livishi, Siha mkoani Kilimanjaro, Wahiyasaa Kihundwa (30), anadaiwa kupoteza maisha baada ya kushambuliwa na tembo wakati akiwa akilinda mazao shambani dhidi ya wanyama hao.

Akizungumzia tukio hilo, baadhi ya wananchi akiwamo Salomon Nkini, alisema kutokana na kukithiri kwa tembo hao katika maeneo ya mashamba na kufanya uharibifu, walilazimika kuweka ulinzi ili kunusuru hasara.

"Usiku wa kuamkia Agost 8, mwaka huu, nilipigiwa simu na walinzi wengine waliokuwa wanalinda shamba langu kwamba kuna mlinzi amepoteza maisha baada ya kushambuliwa na tembo. Nilifanya jitihada za kwenda shambani na kuwasaidia waliobaki pamoja na kuongeza nguvu za kuwafukuza waliobaki," alisema.

Alisema kundi la tembo kutoka msitu wa asili wa Kilimanjaro liliingia kwenye mashamba ya wakulima eneo la Pongo na walinzi walichukua jukumu la kupiga kelele za kuwafukuza na walionyesha dalili za kuondoka, ghafla mmoja aliyekuwa na mtoto aligeuka nyuma na kuanza kuwafukuza.

"Mara baada ya tembo huyo mwenye mtoto kuanza kuwakimbiza, marehemu aliishiwa nguvu na kuanguka ambapo tembo huyo alimshambulia na kisha kuondoka zake," alisema Nkini.

Naye Maria Ndosi, alisema tembo hao wameendelea kuwa tatizo hasa nyakati za kuvuna na kuiomba serikali kuongeza nguvu ya kuwafukuza ili kuepusha madhara yatakayoweza kujitokeza yakiwemo ya watu kupoteza maisha pamoja na tatizo la njaa.

"Kwa sasa hakuna kulala, makundi ya tembo yamekuwa yakishuka kwa wingi na kufanya uharibifu mkubwa bila fidia yoyote. Tunaomba serikali kuongeza wataalamu katika kuhakikisha wanawafukuza wanyama hao pamoja na kulipa fidia kwa wakulima wanaopata hasara kutoka na wanyama hao, "alisema Ndosi.

Elisante Mfoi alisema hasara na vifo vitokananyo na wanyama hao vinachangiwa pia na maofisa wanyapori kuchelewa kuwajibika mara wanapopewa taarifa juu ya uwepo wa makundi hayo ya tembo kwenye mazao jambo ambalo wananchi wanaamua kuingia na kuanza kufanya kazi wenyewe.



Katibu Tawala Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Juma Mfaki (kulia), akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Muheza, alipokuwa akikagua ujenzi wa miundombinu ya shule hiyo hivi karibuni. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Tembo waharibu ekari 28 za mahindi

**Na Cynthia Mwilolezi**, SIMANJIRO

WAKULIMA wa Kata ya Msitu wa Tembo, Simanjiro mkoani Manyara, wameharibiwa ekari 28 za mahindi, baada ya tembo kuvamia kwenye mashamba yao.

Diwani wa Msitu wa Tembo, Kaleiya Mollel, akizungumza jana kwenye kikao cha baraza la madiwani kilichofanyika kwenye Mamlaka ya Mji Mdogo wa Orkesumet ameiomba serikali ichukue hatua.

Mollel alisema tembo hao wamevamia mashamba ya wananchi wa eneo hilo na kuharibu mazao, hivyo kusababisha wakulima kupata hasara ya ekari 28 za mahindi. "Tembo hawatosheki hata ekari 500 hazitawatoshi. Sasa ili kubakisha kile kilicholimwa tunaomba tembo hao waondolewe kwenye eneo la kata yetu," alisema Mollel.

Pia alisema serikali inapaswa kuingilia kati suala hilo kwa kuwa wakulima watakumbwa na njaa kwa sababu ya kukosa mavuno.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Gracian Makota, alikiri kuwapo kwa tembo kwenye baadhi ya kata hiyo. "Tuko kwenye mpango wa kumaliza kero na changamoto hiyo ya tembo kwa kuwafundisha wana vijiji namna ya kuwafukuza shambani tembo hao," alisema Makota.

Naye Kaimu Ofisa Maliasili Halmashauri hiyo, Joseph Shamba, alisema wameandaa mpango wa kuwafundisha vijana wa maeneo husika ili wawafukuze tembo hao. Shamba alisema kata zenye changamoto kubwa waandae vijana 10 au 30 kwenye vijijini, ili watengeneze mabomu kupitia fataki na tochi zenye mwanga mkali.

"Tunaanza na Kata za Msitu wa Tembo, Loiborsoit, Ngorika na Edonyongijape kwa kuwa ndizo zimeathirika mno, kisha maeneo mengine yatafuata", alisema Shamba.

# Waokolewa katika hatari kufanyiwa ukatili

**Na Allan Isack**, ARUSHA

WATOTO 11 wenye umri chini ya miaka 18 waliokuwa hatarini kufanyiwa ukatili wa kijinsia wamenusurika kukumbana na tatizo hilo huku wakisaidiwa kuendelea na masomo shuleni mahali salama pa kuishi.

Hayo yalisemwa jana jijini Arusha na Rose Njilo, Mratibu wa Shirika la Mimutie Women Organization (MWO), aliyasema hayo jana jijini hapa wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Watu wa Asili Duniani ambayo yaliratibiwa na shirika hilo.

Alisema kuanzia Januari, mwaka huu, wamewanusuru watoto 11 ambao walikuwa tayari kuozeshwa kwenye umri mdogo.

Pia alisema shirika hilo limefanikiwa kwa takribani asilimia 75 kupambana na ukatili wa kijinsia kwa watoto na wanawake hasa ndoa za umri mdogo na mimba za utotoni.

Alisema katika mapambano hayo wameanzisha kituo kwa ajili ya manusura wa ukatili wa kijinsia ambacho kimetokana na elimu na uhamashishaji kwa jamii kuripoti matukio ya ukatili wa kijinsia.

"Sasa hivi kama taasisi tumekuwa tukipokea kesi mbalimbali ikiwamo za wanawake kupigwa, kuteswa na kunyang'anywa ardhi kwa kuwa ni wajane au kutopata mtoto wa kiume. Lakini pia kabla ya kuanzisha kituo hiki manusura wa ukatili waliporipotiwa tulikosa sehemu salama za kuwapeleka," alisema.

Pia alisema wamefanikiwa kuwasaidia watoto wakike ambao wengi wao kwa sasa wako shuleni wanasoma kwa ngazi mbalimbali za elimu ili kufikia malengo yao.

Alitoa rai kwa jamii za asili hasa za pembezoni kutumia njia wanazotumiaga kila siku kutatua migogoro katika jamii.

"Vyombo hivyo vya asili ni pamoja na viongozi wa kimila kwa (Laigwanani) na (Ingaigwanak) kwa wanawake kupaza sauti na kuondoa na kutokomeza mila zote kandamizi.

Naye Iddi Ninga, kutoka katika Mtandao wa Mashirika ya Kupinga Ukatili wa Kijinsia katika Jamii za Pembezoni, alisema katika kuadhimisha siku hiyo, wametoka na mapendekezo mbalimbali ambayo yakitumika yatasaidia kutokomeza ukatili huo.

Alisema kuna mbinu mbalimbali za asili ambazo zinakwenda sambamba na utamaduni kwenye jamii hizo, kwa kuwa zikitumika vema zinaweza kuwa msaada wa kutokomeza ukatili huo.

Neema Laizer, mkazi wa Simanjiro mkoani Manyara, akisoma taarifa fupi kwenye maadhimisho hayo, aliomba serikali kutambua sheria na hukumu za viongozi wa kimila kama sheria za asili ili kutatua migogoro bila ya kuathiri nchi.

Pia alipendekeza kuwapo na shughuli za kitamaduni za kuhamasisha kupinga ukatili wa kijinsia ikiwamo 'Alamal' kadhalika mila kandamizi na uongozi ziwe mila shirikishi kwa wanaume na wanawake ili kuweka usawa wa kijinsia.

"Tunaomba serikali, ili itambue kisheria na kisera jamii hizi asili pamoja na maeneo yao kwa kuwa wanawake na watoto wapate utulivu na maendeleo, lakini pia serikali iweke huduma muhimu za kibinadamu katika jamii za asili,"alisema.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Vituko vya Dk. Remmy na gari yake mitaani

## - Aiwekea nembo 'baba yako analo?'; watoto lifti bure

**Na Adam Fungamwango**

TUMESHAWAHI kwenye safu hii hivi karibuni kumzungumzia mwanamuziki maarufu nchini Tanzania, Dk. Remmy Ongalla, jinsi alivyokata rufaa baada ya kupigwa mweleka kwenye mashindano ya mtu mwenye sura mbaya yaliyofanyika mwanzoni mwa miaka ya 1990.

Remmy, ambaye jina lake halisi ni Ramadhani Mtoro Ongalla aliyezaliwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, wakati huo ikiitwa Zaire, licha ya kwamba alikuwa ni mwanamuziki mkubwa na maarufu, akiimba nyimbo mbalimbali zilizopendwa, na kuchukua tuzo, lakini pia alikuwa ndiye mwanamuziki mwenye vituko zaidi nchini Tanzania kwa wakati huo.

Akishirikiana na wenzake, walianzisha mashindano ya mtu mwenye sura mbaya yaliyofanyika kwenye ukumbi mmoja Buguruni na kugaragazwa vibaya na kijana mmoja aitwaye Masudi, ambaye baadaye alitambulika zaidi kwa jina la Masudi Surambaya.

Remmy alishika nafasi ya pili na mwigizaji maarufu wakati huo, Bakari Mbelemba, maarufu kama mzee Jangala akakamata nafasi ya tatu.

Remmy, ambaye alijua atashinda kirahisi pambano hilo, hakukubali, akakata rufaa kwa majaji kuwa mshindi wa kwanza Masudi hakuwa mbaya wa asili, bali ulitokana na kuugua ukoma.

Majaji waliichukua rufaa yake na kuifanyia kazi. Kilichotokea ni kwamba rufaa ya Remmy ilitupwa, kwani ilionekana Masudi yuko vile tangu utoto wake.

Kilichomuuma zaidi Remmy ni vyombo vya habari, hususani magazeti wakati ule kuandika, Remmy pamoja na ubaya wake, lakini kwa Masudi alionekana mrembo tu.

Ilimuuma sana kwani aliamini hakuna mtu mwenye sura mbaya nchini Tanzania kama yeye, na akaimba nyimbo nyingi za kujisema kama yeye ni mbaya kama 'mtoto ni mtoto kwa mama hakui, hata kama angelikuwa kilema au mbaya kama Remmy, ni mtoto tu.' Wimbo huo unaitwa 'Nalilia Mtoto' Wimbo mwingine ni 'Mnyonge hana haki', kuna kipande anaimba 'Remmy myonge, Remmy sura mbaya, Remmy hana la kusema mbele ya wenzake.'

Alijitahidi sana kutaka kuandaa tena mara ya pili kwani alijua atashinda, lakini ilishindikana kwa sababu alianza kuugua na alipopona, akaamua kuokoka.

Ila cha ajabu ni kwamba, pamoja na kumkatia rufaa, lakini Remmy alianza kumtumia Masudi Surambaya kwenye maonyesho yake.

Sitaki kuendelea sana na hili kwa sababu tayari tumeshalizungumzia, ila nimegusia kumuonyesha Remmy jinsi alivyo nje ya muziki.

Ni mtu mwenye vituko, na anapopita iwe kwa miguu au ndani ya gari, lazima watu wajue kama anapita.

Mavazi yake, nywele zake aina ya rasta, zilikuwa kivutio ukichanganywa na umaarufu wake ndiyo kabisa. Ndiyo maana kuna wimbo aliimba, 'Remmy akipita barabarani watoto humfuata'. Ni kweli kabisa.

Hakuwa mtu wa majivuno, alikuwa rafiki na kipenzi wa kweli wa mashabiki, kwani wao walimpa upendo na yeye akalipa kwa kuwapa faraja kwa kuongea na kucheka nao.

Kituko ambacho hakijawahi kuelezewa sana ni gari lake. Sijui alilinunua kwa bahati mbaya au makusudi ili tu avunje mbavu watu. Muundo wa gari ile sina uhakika nayo kama ilikuwa ni 'Morris' au 'Austin', yale magari ya kizamani kabisa, ambayo kwa miaka ya 1980, yalionekana yamepitwa na wakati. Ni kipindi Tanzania ilishuhudia magari mapya kama Renault na Peugeot, hasa 504 maarufu kama 'guruwe' ndiyo yalikuwa yameingia na ndiyo ya kisasa.

Gari la Remmy likionekana barabarani linaonekana ni kituko, na yoyote anayeliona ataanza kulishangaa kwa kukodolea macho au kucheka. Mwenyewe alijua hilo. Nyuma ya gari hilo aliandika maandishi yaliyosomeka 'Baba yako analo?' Unapolicheka, ukisoma maandishi nyuma, utaacha kucheka na kujiuliza maswali, au utazidi kuvunjika mbavu kutokana na kushuhudia kichekesho juu ya kichekesho.



Aliyekuwa mwanamuziki maarufu nchini, Hayati Dk. Remmy Ongalla aliyezaliwa Februari 10, 1947 Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.



Gari aina ya Morris Minor lililotengenezwa nchini Uingereza kuanzia miaka ya 1948 hadi mwaka 1952. Ndiyo aina ya gari alilokuwa nalo mwanamuziki Dk. Remmy Ongalla ambapo miaka ya 1980 lilionekana limepitwa na wakati na yalikuwa adimu sana barabarani kiasi kwamba inakuwa kama kioja likionekana mitaani.

Baadaye alinunua gari lingine halitofautiani sana na hilo, lakini akaandika 'sukari imeingia sumu, mambo kwa soksi.' Yalikuwa ni maandishi yaliyowatahadharisha watu kuhusu ugonjwa hatari wa ukimwi, wakati huo ndiyo ulikuwa umeingia na wengi hawana uelewa.

Alikuwa akiwakumbusha juu ya kutumia mipira ya kiume.

Kwa upande wa watoto walimpenda Remmy kwa sababu alikuwa akiwapa sana lifti kwenye gari lake, hapo na mimi si haba ni miongoni mwa wanufaika wa lifti hiyo, Mungu ambariki alikotangulia.

Akipita kituoni na kukuta wanafunzi hasa watoto kuanzia wanaosoma chekekea na shule za msingi, atasimama na kuwapakiza mpaka gari lake lijae. Yeye huwaambia 'Pandeni niachieni kiti changu tu'. Hiyo ilikuwa ndiyo tabia yake popote pale anapopita. Kumbuka watoto hawa huwa wanakwenda kuwaambia wazazi wao majumbani juu ya kupewa lifti naye. Ndiyo maana umaarufu wa Remmy ulikuwa mkubwa maradufu. Siyo kwa ajili ya muziki tu peke yake. Roho yake ya upendo, huruma, ukarimu, kujiweka karibu na mashabiki wake, kutokuwa na maringo, licha ya kuwa ni staa mkubwa ndani na nje ya nchi, ilimfanya kupendwa na kuheshimiwa zaidi.

Mwanamuziki huyo alifariki Desemba 13, 2010 na kuzikwa kwenye makaburi ya Sinza, eneo ambalo alipokuwa akiishi tangu kukiwa pori mwanzoni mwa miaka ya 1980, kiasi kwamba hadi leo sehemu hiyo imepewa jina lake kwa heshima yake tangia yupo hai hadi alipofariki 'Sinza kwa Remmy'.

Hata uamuzi wa maziko yake Sinza Makaburini, kamati ya mazishi ilipendekeza kuenzi umaarufu na aliyotendea eneo hilo.

**Kwa maoni tuma 0716 350534**

# Ecowas yaamuru jeshi kuivamia Niger

**ABUJA, Nigeria**

NCHI zinazounda jumuiya ya ushirikiano wa Afrika Magharibi (ECOWAS) zimeidhinisha kuchukuliwa hatua ya kijeshi kuwaondoa viongozi wa kijeshi nchini Niger.

Hatua hiyo inachukuliwa kama njia ya kumrudisha madarakani Rais Mohamed Bazoum ambaye alipinduliwa wiki chache zilizopita.

Taarifa ya jumuiya hiyo ilieleza kwamba inaweka tayari kikosi cha jeshi kitakachofanya operesheni nchini Niger ili kurejesha utawala unaotambulika kikatiba.

Rais wa Nigeria Bola Tinubu ambaye ni mwenyekiti wa jumuiya ya ECOWAS, alisema matumizi ya nguvu za kijeshi itakuwa njia ya mwisho.

Rais wa Ivory Coast Alassane Outarra, alisema takriban wanajeshi elfu moja wa nchi yake watajiunga na kikosi hicho.

Wiki iliyopita, Senegal, Benin na Ivory Coast zilijitolea kupeleka wanajeshi iwapo jumuiya hiyo ya kikanda itaamua kuingilia kijeshi nchini Niger.

Kamishna wa ECOWAS wa Masuala ya Kisiasa, Usalama na Amani, Abdel -Fatau Musah aliambia BBC kwamba wanajeshi watapelekwa nchini humo wakati wowote.

"Hatutafanya mazungumzo milele. Operesheni hiyo itasitishwa tu ikiwa mamlaka ya kijeshi ya Niger itaamua kufanya mazungumzo ya kumrejesha madarakani Rais Bazoum na kuirejesha nchi kwenye utawala wa kikatiba." Alisema Musah.

Kamishna huyo pia alidokeza kuwa Rais Bazoum alikuwa akiishi chini ya mazingira yasiyo ya kibinadamu baada ya kukataa kwake kutia saini hati za kujiuzulu.Jumuiya ya ECOWAS ililaani mapinduzi hayo na kuendelea kuzuiliwa kwa Rais Bazoum, ikisisitiza kuwa haitaomba msaada kutoka nje katika kushughulikia mzozo wa kisiasa wa Niger.

**BBC**



Miji ya Ukraine imekuwa ikishuhudia mashambulizi ya kila wakati tangu Russia ilipotuma vikosi vyake zaidi ya mwaka mmoja uliopita. Pichani ni kikosi cha uokoaji kikitafuta waathirika katika mji wa Kyiv. **PICHA: XINHUA**

# Moto umesababisha vifo vya watu 55 Marekani

**WASHINGTON,** MAREKANI

MOTO unaoendelea kuwaka katika misitu ya Hawaii nchini Marekani, umesababisha vifo vya watu 55 na idadi inaweza kuongezeka kutokana na watu wengine kupotea.

Maofisa wa Hawaii walisema moto huo ni miongoni mwa majanga mabaya zaidi kuwahi kushuhudiwa katika historia ya jimbo hilo la Marekani. Kwa mujibu wa maofisa hao wa Kaunti ya Mauim wazima moto wanaendelea kupambana kuuzima moto huo.

Rais wa Marekani, Joe Biden ametangaza moto huo kuwa janga na kuidhinisha msaada wa shirikisho kwa ajili ya shughuli za uokozi na kiutu.

Moto huo unafuatia matukio mengine mabaya ya hali ya hewa katika Amerika ya Kaskazini wakati wa majira ya joto.

Moto huo wa msituni umevunja rekodi kuteketeza kilomita nyingi kutoka Canada hadi Marekani. Ulaya na maeneo mengine ya Asia pia yameshuhudia kupanda kwa viwango vya joto.

**DW**

# Israel yawaondoa raia wake Ethiopia

**ADDIS ABABA**

Israel imetangaza kuwa imewaondoa kwa ndege maalum zaidi ya raia wake 200 wakiwamo Wayahudi wenye asili ya Ethiopia kutoka miji miwili ya Amhara na Oromia.

Hatua hiyo imechukuliwa baada ya ghasia kuenea katika miji hiyo, raia hao walipelekwa mji mkuu wa nchi hiyo Addis Ababa kwa ajili ya usalama wao.

Mkoa wa Amhara wanaishi maelfu ya watu wa jamii ya Kiyahudi. Katika taarifa yake Waziri Mkuu, Benjamin Netanyahu alisema ameagiza watu waliohamishwa katika maeneo ya mapigano na kwamba wataondoka wote kuelekea Israel.

Hata hivyo, hali ya utulivu imeripotiwa kuendelea katika miji mikubwa kwenye eneo la Amhara, huku maeneo mengine kukiwa na makabiliano makali kati ya jeshi na wanamgambo wa eneo hilo.

Jeshi la serikali lilisema lilipata udhibiti tena katika mikoa muhimu lakini baadhi ya wakazi kutoka miji midogo walisema wanamgambo wa eneo hilo bado wanadhibiti.

Wakati huo huo Marekani na Uingereza zimeungana na nchi nyingine tatu Japan, Australia na New Zealand kuelezea wasiwasi wao kuhusu kuzorota kwa usalama nchini Ethiopia.

Taarifa ya pamoja iliyotolewa jana ilisema ghasia za hivi karibuni katika mikoa hiyo imesababisha vifo vya raia na uharibifu wa mali.

Tume ya Umoja wa Mataifa ya Wataalamu wa Haki za Kibinadamu nchini Ethiopia hapo awali ilisema imesikitishwa na hali ya ukosefu wa usalama na kuitaka serikali kuzingatia kanuni, uwiano na kutobagua katika kutekeleza hali ya hatari iliyotangazwa nchini humo.

**BBC**

## Russia, Ukraine zashambuliana

**KYIV,** UKRAINE

MILIPUKO kadhaa imesikika kwenye maeneo ya mji mkuu wa Ukraine, Kiev, baada ya kutangazwa tahadhari ya mashambulizi ya anga nchini nzima.

Maofisa wa Ukraine walisema kikosi cha anga kilikuwa kazini na kiliripoti kuwa Russia ilifanya mashambulizi ya makombora ya mwendo wa kasi kwenye mji huo.

Maofisa hao walisema vipande vya kombora lililodunguliwa vimeanguka kwenye eneo la hospitali ya watoto, lakini hakuna watu waliojeruhiwa wala kufanya uharibifu.

Aidha, Russia ilisema imeiharibu ndege isiyo na rubani ya Ukraine katika viunga vya mji wa Moscow.

Wizara ya ulinzi ya Russia ilisema jaribio la Ukraine kufanya shambulizi la kigaidi limeshindikana.

Wakati huo huo, mji wa kihistoria wa Ujerumani wa Wurzburg, umetoa magari matatu ya kikosi cha zima moto kwenda Lviv, baada ya kombora kutoka Russia kuushambulia mji huo.

**DW**

## Wanajeshi 23 wauawa Syria

**DAMASCUS,** SYRIA

WATU wenye silaha wamelishambulia basi lililowabeba wanajeshi wa Syria na kuwaua askari 23.

Shirika linalofuatilia haki za binadamu nchini Syria, limesema shambulizi hilo limetokea jana asubuhi katika mkoa wa Deir Al Zour.

Katika tukio hilo la kushtukiza wanajeshi wengine 10 walijeruhiwa.

Inadaiwa kuwa shambulizi hilo limefanywa na wapiganaji wa kundi linalojiita Dola la Kiislamu, IS.

Hata hivyo, hakuna maelezo yoyote ambayo yametolewa na IS wala serikali kuhusu mauaji hayo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA PASSPORT YA KUSAFIRIA



**RUTH JIMMY MASAWE** anatangaza kupotea kwa passport ya kusafiria yenye namba **TAE 343836** iliyotolewa DAR ES SALAAM PCO mwaka 2020. Kwa yeyote atakeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **KAT/MPA/RB/267944/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MOHAMED SHABANI MOHAMED** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA CARINA** yenye usjaili namba : **T489 CPF.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/CHU/RB/270008/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**NUHU ROBERT KAFYULILO** Anatangaza kupotelewa na kadi ya **BAJAJI (TVS KING)** yenye namba za usajili **MC 564 CSA** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi **DSM/PHQ/RB/264960/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**OBADIAH MATHEW MKILANYA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA HARRIER** yenye usajili namba: **T 742 CQE,** CHASSIS NAMBA: **SXU150007058** na ENGINE NAMBA: **5SDB12740.** Kwa yeyote atakaeiona atoe tarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **ARU/ARU/RB/269370/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**WILAYA YA MOROGORO**
**KITUO CHA MJINI, MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na......77/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: PETRO RUBEN RITE wa Mwembesongo**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOTOLEWA NA CAROLINA PATRICE SENGE**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 23 Mwezi 08 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Zingatia;
- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

Imetolewa leo tarehe 02 mwezi 08 mwaka 2023

**G.A.NG'ITU**
..............................................
**HAKIMU**

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**LEGENDS AUCTION MART AND GENERAL BROKER LIMITED** Kwa Idhini na Mamlaka tuliyopewa na **MAENDELEO BANK PLC** tunatoa notisi ya **SIKU KUMI NA NNE (14) TU, YA KULIPA DENI UNALODAIWA** kuanzia siku ya tangazo hili,Vinginevyo, tutafanya mnada wa hadhara wa kuuza DHAMANA ulizoweka kwenye mkopo kama ratiba inavyoonyesha.

| S\N | JINA LA MDAIWA\MDHAMINI | DHAMANA MAHALI ZILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1. | EAG GROUP LIMITED | Commercial building, plot no 1094, block m, forest area, mbeya city | 29\08\2023 Kuanzia saa 4:00 asubuhi na kuendelea. |
| 2. | MIDIAM BEATUS KINGWILE | Kiwanja chenye hati na.18147-MBYLR-Mbeya-Iteza. | 01/09/2023 Kuanzia saa 4:00 asubuhi na kuendelea. |
| 3. | MOHAMED SADIKI SIMBA | Gari-T693 DCA-Verosa. Iliyopo Dar es Salaam-Posta House. | 04/09/2023 Kuanzia saa 4:00 asubuhi na kuendelea. |
| 4. | ANTUSER JUNIEL LEMA | Gari-T504 DBS-Toyota NOAH. Iliyopo Dar es Salaam-Posta House. | 21/08/2023 Kuanzia saa 4:00 asubuhi na kuendelea.(Marudio). |

**MASHARTI YA MNADA**
1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
3. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwishailipa.
4. Gharama zote za kubadili hatimiliki ni za mnunuzi
5. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no. **0714939933/0713857349**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**

**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI 198LA 2022**

**CECY MICHAEL YASINI...............MUOMBAJ/WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

**GIBSON MWAGONELA....................MDAIWA/WADAIWA**

**WITO KUIOTWA SHAURINI**

**GIBSON MWAGONELA**
**POPOTE ULIPO/MLIPO**

**CECY MICHAEL YASINI** amefungua shauri mbele ya baraza la ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (Mwananyamala) Shauri husika limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 4/9/2023 saa 03:00 asubuhi/mchana mbele ya Mh J.W. SILLAS Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe **09 Mwezi 08, 2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA WILAYA YA MOROGORO**

**MKOA WA MOROGORO**

**KATIKA SHAURI LA MADAI NA. 22/2021**

**JUMA LUKINDA MAJEGELO: ................................MDAI**

**DHIDI YA**

**PATHEC LIMITED: ........................................MDAIWA**

**WITO/KUITWA SHAURINI**
**PATHEC LIMITED**
**POPOTE ULIPO**

Unatakiwa ufike katika Mahakama ya Wilaya Morogoro tarehe 18/8/2023 saa 2:30 asubuhi ambapo shauri lako limepangwa HUKUMU.

Endapo hutofika wewe binafsi ama mwakilishi wako shauri tajwa litasikilizwa upande mmoja na kutolewa uamuzi.

**Imesainiwa leo tarehe 11 mwezi AUGOST mwaka 2023**

HAKIMU MKAZI MFAWIDHI
MOROGORO.

**BARAZA LA KATA SINONI**
**OFISI YA BARAZA KATA YA SINONI**
**ARUSHA**

**WITO KWA:**
1. **First World Investment**
2. **Patricia Ismael Matogo**
3. **Mohamed Farari**

Wa Mtaa wa............. kata ya ......... unajulshwa/mnajulishwa kuwa leo Tarehe 01/08/2023 umelalamikiwa/mmelalamikiwa na Patrick Swai kuwa nyumba yake ya wapangaji imefungwa bila idhini ya yake na wapangaji wake wanaendelea kupata usumbufu.
Kwa wito huu baraza hili la kata ya Sinoni Jijini Arusha linakuita uwepo Tarehe 15/08/2023 ili uweze kujibu tuhuma/lalamiko hilo
Hakikisha unahudhuria mbele ya baraza hili bila kulazimishwa saa 4:00 Asubuhi Jumanne
Ofisi ya Baraza letu iko ndani ya jengo la Ofisi ya A/Mtendaji kata ya Sinoni karibu na Kanisa Katoliki Jimbo Kuu Arusha wa Mlimani Sinoni
**Mawasiliono : 0678-015730/ 0755-015830**
Kwa wito huu fikeni saa iliyopangwa bila kuchelewa. Hatua kali zitachukuliwa msipofika.

...........
**BARAZA LA KATA YA SINONI**
**ARUSHA**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710. E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

***Uza,***
***Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi***
***Kwa Bei Poa. Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MBWA mmoja wa jirani wa maeneo ya Kinondoni Msisiri, alionekana kuvutiwa na kiroba kilichotupwa upenuni mwa nyumbani moja. Ni moja kati ya viroba ambavyo hutupwa usiku au alfajiri na vijana wanaokusanya taka kwenye nyumba za watu na kupewa ujira kidogo. Wao badala ya kwenda kutafuta maeneo ya kutupa, hupita vichochoroni na kama hajaonekana anautupa mzigo na kuendelea na safari yake. Ilitokea kwenye nyumba moja huko, na mbwa huyo alipouvuta, kiungo vya mwili wa bianadamu vilianguka. Majirani a kwanza kuona walipiga kelele na watu wakajazana. Akinamama wakiangua vilio. Viungo vilihifadhiwa kwa kufunikwa. Polisi walianza msako. Kwa kuanzia tu wakaanza kuwakamata wazoa taka na waokota chupa za kwenda kuuza, wote wa maeneo hayo na jirani wanaofahamika tayari kwa mahojiano na uchunguzi, wakihisiwa kuwa huenda mmoja wao au zaidi kuhusika na mauaji. Ni maiti ya nani? Na Muuaji ni nani? Fuatilia mwanzo hadi mwisho kujua mkasa mzima ulivyokuwa.

# Maiti kwenye kiroba-21

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

Baada ya kuona kimya sana kama nipo peke yangu, halafu nikawa nashangaa nyumba kubwa na nzuri kama ile kuwa haina mtu, nikanyanyuka na kwenda uani ambako niliona wameelekea."

"Uliwakuta?"

"Nilipofika uani mbele ukumbi mdogo hivi, nikaingia, pembeni kulikuwa na vyumba. Ghafla nilifika kwenye dirisha ya chumba kimoja kinaona kitu cha ajabu."

"Kitu gani?"

"Nikamuona mwanamke alikuwa amefungwa mikono na miguu, amefungwa na kitambaa mdomoni, halafu yule mwenyeji wetu akawa na kisu kikubwa, akawa anamfungua miguu na mikono, akaanza kumkata mkono mmoja mmoja mwanamke yule akiwa hai. Mwanamke alionekana kuwa na maumivu makali lakini mwili wake ulikuwa umefungwa kwenye nguzo. Hakuweza kufanya chochote akiwa na wanaume wake wawili."

"Anko wako yeye alikuwa anafanya kitu gani?

"Alikuwa kama msaidizi, na yeye alikuwa anafanya kazi hiyohiyo ya kukata viungo. Nilichogundua ni kwamba yule mwenyeji wetu alionekana kuwa na hasira na yule mwanamke lakini alikuwa mwoga, ila anko wangu ndiye aliyekuwa akimwekeza cha kufanya, na alionekana ni mzoefu na katili sana, inaonekana ndiyo kazi zake na amechukuliwa kwa kazi hiyo ingawa mimi sikuwahi kufikiri kuwa yuko hivyo.

Ila samahani kidogo, kabla ya kumkatakata walimfanyia ukatili mkubwa. Kusema kweli nilikuwa sijawahi kuona kitu kama hicho maishani. Nilitamani nipige kelele lakini nikaona na mimi itakuwa ni mwisho wangu hapa, nilichofanya niliimana ili nisionekane halafu nikatoka mbio kurudi nilipokuwa mwanzo."

"Walirejea baada ya muda gani?"

"Baada ya saa mbili tangu nilipowaona walirejea. Wakaniomba radhi kwa kuchelewa, wakasema wao ni wafanyabiashara wana mzigo wanataka kuusafirisha mzigo kwa hiyo niwasaidie kuubeba. Wakasema walichelewa kwa sababu walikuwa wanafunga bidhaa hiyo vizuri kwa sababu ni ya magendo hivyo hawataki trafiki au askari wengine walione."

"Kwa hiyo wewe ndiye uliyeubeba?"

"Ndiyo, walipoutoa ndani mimi ndiyo niliyeubeba hadi sehemu fulani tukakodisha bajaji hadi karibu na kituo cha Banana. Tukateremka na kuanza kutembea tena kwa miguu mzigo ukiwa kichwani mwangu."




**"Baada ya saa mbili tangu nilipowaona walirejea. Wakaniomba radhi kwa kuchelewa, wakasema wao ni wafanyabiashara wana mzigo wanataka kuusafirisha mzigo kwa hiyo niwasaidie kuubeba. Wakasema walichelewa kwa sababu walikuwa wanafunga bidhaa hiyo vizuri kwa sababu ni ya magendo hivyo hawataki trafiki au askari wengine walione."**

"Unaweza kujua ulikuwa mzigo wa nini?"

"Kwa wakati huo nilikuwa sijui, ila kwa picha niliyoiona nilikuwa kama nahisi kuwa inawezekana ikawa ni maiti ya yule dada kwani nilikuwa na uhakika kuwa watamuua, ila uhakika kuwa waliitoa maiti kwa staili ile sikuwaza, ila baadaye sana ndipo nilipotambua."

"Mliipeleka wapi?"

"Tulipofika Banana yule mwenyeji wetu akatuambia tusubiri amempigia simu dereva wake anakuja. Akafika jamaa mmoja dereva taxi wa uwanja wa ndege ambaye huwa anamchukua mara kwa mara, tuseme ni kama dereva wake kila anapomhitaji. Mzigo tukaupeleka Magomeni Mikumi."

"Ulipaona walipouingiza?"

"Kusema kweli hapana. Tulifika Magomeni Mikumi kituoni, nikaushusha mimi mwenyewe, halafu anko wangu akabaki na mwenyeji, dereva akaambiwa anipeleke nyumbani Manzese."

"Baada ya hapo hakuna kitu kingine unachojua?"

"Ndiyo!"

"Okay tunaweza kumpata huyo anko wako?"

"Hata sasa hivi naweza kuwapeleka."

"Anaitwa nani Anko wako?

"Tinga Patauli."

Eddy aliwaita wasaidizi wake na kumuondoa Mboneka, kisha akampigia Inspekta Frank.

"Afande naomba wasaidizi wako waje kumchukua huyu jamaa, halafu wafanye hila na kumkamata mtu mmoja anaitwa Tinga Patauli. Huyu akikamatwa naomba muwakabidhi wasaidizi wangu, ni mtu muhimu sana kwenye upelelezi huu."

"Okay Eddy haina tatizo, nadhani sasa mambo yamekuwa bambam."

Eddy akacheka kidogo, halafu akamwambia "Kesi imeisha hii, wauaji wameshajulikana."

"Ni mmoja au wengi?"

"Bado sijajua, ila kwa sasa nachokusanya mimi hapa ni ushahidi tu ili tukiwatia mbaroni kila kitu hadharani."

"Okay, sasa tukamkamate huyo Tinga?"

"Anaonekana ni mjanja mjanja, huyu anatakiwa mumtumie ndugu yake Mboneka ili kumkamata. Ajifanye ana shida fulani ambayo inahitaji yeye aende sehemu. Kuwe na askari kanzu pembeni ambao watamtia mbaroni akifika hapo."

"Okay Eddy, tutakachofanya tutatengeneza ajali bandia ambayo mtuhumiwa atakuwa ameipata kwa sababu mpaka sasa hajui kama amekamatwa. Baada ya kutengeneza, tutamwambia ampigie simu ili aje na hapo ndipo tutaifanya hiyo kazi, sawa bwana Eddy?"

"Nadhani kazi hapo imekwisha."

"Nakutakia maendeleo mema ya kazi."

"Yaani wiki haiishi, kila kitu kitakuwa sawa." Eddy na Inspekta Frank wakamaliza mazungumzo.

********************************

"Hallow mzee Voley habari yako?"

"Nzuri mheshimiwa za huko?"

"Safi, naomba nisaidie kitu kimoja."

"Ndiyo mheshimiwa nakusikia."

"Kati ya yale majina uliyonipa ni nani ambaye ana nyumba kule Ukonga Banana?"

"Charton Antony ndiye mwenye nyumba Ukonga." Halafu akauliza 'Kwani vipi?"

"Hapana, nauliza tu nipate kujua kwa sababu za kikazi."

"Ndiyo hivyo ana nyumba Gongolamboto na nyingine ipo Ukonga Banana, lakini hiyo amempangisha mtu na familia yake."

"Okay, basi nitakutafuta mara nyingine."

"Karibu tena."

Ni mazungumzo ya simu kati ya Eddy na Peter Voley. Huyu ni mjomba wa marehemu Tessy aliyeuawa kikatili kwa kukatwakatwa mapanga na mabaki ya mwili wake kuwekwa kwenye kiroba.

Ni yeye ndiye awali aliyempa majina ya watu wengi ambayo Eddy Kamal aliyahitaji kwa ajili ya kuanza kufanya upelelezi.

Aliomba majina ya ndugu kadhaa wa marehemu, mashoga zake, na watu wengine ambao aliona anaweza kuanzia upelelezi hapo.

Kitu kilichoanza kumtatiza na kumchanganya hapo ni kuwa, je Charton Antony ndiye aliyekuwepo siku hiyo kwenye nyumba ya Ukonga Banana akawakaribisha Tinga na Mboneka, au ni mpangaji wake kama anavyodai Voley kuwa alimpangisha mtu mweye familia.

"Je huyo mtu aliyepanga nyumba hiyo ni nani? Na kwa nini aliwakaribisha watu hao wawili na kuonekana anamtesa na kumuua mwanamke?" Akajiuliza Eddy.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# PLUIJM BADO ANALIOTA BAO LILILOKATALIWA MKWAKWANI

**Na Faustine Feliciane, TANGA**

KOCHA Mkuu wa Singida Fountain Gate, Hans van der Pluijm, amesema kwa mtazamo wake na sehemu aliyokuwa amesimama, goli lililokataliwa katika mechi yao dhidi ya Simba lilikuwa halali.

Simba ilitinga hatua ya fainali ya michuano ya Ngao ya Jamii kwa ushindi wa penalti 4-2, timu hizo zikitoka suluhu katika dakika 90 za kawaida.

Akizungumza na gazeti hili jana, Pluijm, alisema timu yake ilicheza vizuri zaidi katika kipindi cha kwanza na anaamini bao lililokataliwa na mwamuzi, Amina Kyando kutoka Morogoro dakika ya saba ya mchezo huo walidhulumiwa.

"Sitaki kuzungumzia sana suala la maamuzi, lakini kwa maoni yangu na eneo nililokuwa nimesimama sikuona sababu ya kulikataa lile goli la Kazadi (Francy), lilikuwa goli halali lakini mwamuzi na wasaidizi wake wao pengine waliona zaidi kutokana na eneo walilokuwa wamesimama," alisema Pluijm.

Aliongeza kiujumla wachezaji wake walicheza vizuri na walikuwa na malengo ya kuifunga Simba ingawa hilo halikuwezekana.

"Nawapongeza sana wachezaji wangu, walijituma sana lakini hatukuwa na bahati na kujikuta tunapoteza mchezo kwa mikwaju ya penati," alisema Pluijm.

Kocha huyo alisema wachezaji wake hawakufanya mazoezi ya kutosha ya kupiga penati na walipofika katika hatua hiyo wachezaji wengi walikuwa wanakataa kuchukua jukumu kutokana na presha ya mchezo.

Hata hivyo Aidha, alisema kwa namna timu yake ilivyoimarika na ubora wa wachezaji wake anauhakika wa kutoa upinzani katika mbio za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Bara msimu mpya.

"Tutakuwa sehemu ya timu zitakazowania ubingwa, nina uhakika tutakuwa bora zaidi katika msimu ujao ukilinganisha na msimu uliopita, naamini ubora wa wachezaji wangu na uimara wa timu," alisema Pluijm.

Singida FG sasa itakutana na Azam FC katika mechi ya kusaka mshindi wa tatu wa michuano ya Ngao ya Jamii utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini hapa na baadaye fainali itakuwa ni kati ya Yanga dhidi ya Simba.




Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza, Mzee Ramadhani Nyamka (kulia), akipokea jezi kutoka kwa Mkurugenzi wa Kampuni ya Usambazaji ya Wakazi, Kelvin Ndawi, kwa ajili ya msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2023/2024. **PICHA: SHUFAA LYIMO**

# Prisons yaahidi mapinduzi Bara

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa timu ya Prisons umesema umeandaa vyema kikosi chao na unaahidi kufanya 'mapinduzi makubwa' katika msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo inatarajiwa kufanyika kuanzia Agosti 15, mwaka huu.

Akizungumza wakati wa hafla ya uzinduzi wa jezi watakazozitumia katika msimu ujao, Kamishna Jenerali wa Magereza, Mzee Ramadhani Nyamka, amesema malengo ya timu yao ni kushika nafasi ya juu katika msimamo wa Ligi Kuu Bara.

Nyamka alisema wamejiandaa kuonyesha soka la ushindani na malengo yao ni kupata tiketi ya kushiriki katika mashindano ya kimataifa hapo mwakani.

"Tumejipanga kufanya mapinduzi makubwa, mikakati tuliyonayo ni kuhakikisha tunapata nafasi ya kushiriki mashindano ya kimataifa mwakani, tunaimani na benchi letu la ufundi," alisema Nyamka.

Aliongeza wamefanya usajili mzuri ambao utawasaidia kupata ushindi katika kila mechi na hawana mpango wa kusajili wachezaji wa kigeni kwa sababu malengo yao ni kusaidia kuinua na kuendeleza vipaji vya nyota wa Kitanzania.

Naye Mkurugenzi wa Kampuni ya Wakazi Supply, Kelvin Ndawi, ambao ndio wamewatengenezea jezi alisema wataendelea kufanya kazi na timu hiyo kwa mkataba wa mwaka mmoja.

"Hizi jezi zina ubora wa hali ya juu, naamini kila shabiki atazipenda, wataingia nazo uwanjani kama sehemu ya kuwapa hamasa wachezaji," Ndawi alisema.

## Mandonga, wenzake washitakiwa TPBRC

**Na Saada Akida, TANGA**

BINGWA wa mkanda wa WBC katika upande wa ngumi na mateke (kick boxing), Emmanuel Shija, ameiomba Kamisheni ya Ngumi za Kulipwa Tanzania (TPBRC), kuangalia upya sheria na kanuni ya mchezo huo.

Hatua hiyo imetokana na baadhi ya mabondia kwa sasa kuonekana wanacheza mapambano mara kwa mara bila kujali afya zao.

Akizungumza na Nipashe jana, Shija alisema mabondia wanatakiwa kujali afya zao kwa kutopanda ulingoni mara kwa mara, kwasababu ni hatari kwa afya zao katika siku za baadaye.

Alisema baadhi ya mabondia wamekuwa wakicheza mapambano kila baada ya kipindi kifupi na kwa kufanya hivyo wanaweza kupata athari mbalimbali za kiafya baada ya kuacha mchezo huo.

"Niwaombe TPBRC kuangalia upya sheria au kutunga sheria nyingine itakayosaidia kupunguza athari hizo kwa mabondia hapo baadaye kwa sababu ngumi ni mchezo wa hatari, sio wa vichekesho, pia ninaiomba serikali iendelee kuwekeza katika mchezo huu ili kuurejesha katika nafasi ya kwanza," alisema Shija.

## JKT Queens kamili kuchuana CECAFA

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI mashindano ya Klabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati kwa wanawake yanatarajiwa kuanza leo, wawakilishi wa Tanzania Bara, JKT Queens, wametamba wako tayari kwa michuano hiyo inayofanyika nchini Uganda.

JKT Queens itaanza kuwania taji hilo linaloshikiliwa na Simba Queens kesho kwa kuwavaa AS Kigali Women kutoka Rwanda.

Mkurugenzi wa Ufundi wa JKT Queens, Bakari Shime, aliliambia gazeti hili jana kambi ya timu yake ilikwenda vizuri na anaamini kama wachezaji wakifuata maelekezo, basi watafanya vyema katika michuano hiyo.

"Kila kitu kimeenda vizuri, watu wa benchi la ufundi wamefanya kila kitu vizuri, wachezaji walikuwa na ari ya kupokea, kwa mtazamo wangu naona timu sasa ipo tayari kwa asilimia 95, vimebaki vitu vichache sana ambavyo naamini vitamalizwa haraka," alisema Shime.

Mabingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake wa Ethiopia, CBE FC itafungua pazia la michuano hiyo leo dhidi ya Buja Queens ya Burundi wakati wenyeji Kampala Queens watawakaribisha Yei Joint Stars ya Sudan Kusini.

## ZISIKUPITE

### MAGUIRE SASA KIMEELEWEKA

KLABU ya West Ham inasubiri uamuzi kutoka kwa beki wa England, Harry Maguire, kuhusu kama atajiunga nao baada ya wagonga nyundo hao kukubaliana ada ya pauni milioni 30 na Manchester United kwa ajili ya mchezaji huyo mwenye miaka 30. **(Mail)**

### TUCHEL AMVUTA KANE

KOCHA wa Bayern Munich, Thomas Tuchel, alimfanya, Harry Kane kuwa chaguo lake namba moja na atashangaa ikiwa nahodha huyo wa England hatajiunga na mabingwa hao wa Ujerumani. (**Telegraph)**

### LUKAKU KUMRITHI KANE

KLABU ya Tottenham Hotspur itafikiria kumnunua mshambuliaji wa Chelsea na Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 30, ikiwa nyota wake, Harry Kane atakwenda Bayern Munich. **(Gazzetta dello Sport)**

### MBAPPE HAONDOKI PSG

MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa 24 amerudia msisitizo wake kwa Paris St-Germain hataondoka katika klabu hiyo msimu huu wa joto kwa hali yoyote na anakusudia kumaliza mkataba wake. **(Le Parisien)**

### CAICEDO AKARIBIA LIVERPOOL

LIVERPOOL sasa inaongoza mbio za kumsajili kiungo wa kati wa Brighton, Moises Caicedo, mbele ya Chelsea na iko tayari kuvunja rekodi ya ada ya uhamisho ya klabu hiyo ili kumnasa mchezaji huyo wa Ecuador mwenye umri wa miaka 21. **(Sports)**

### VERATTI ATAKIWA CHELSEA

CHELSEA inavutiwa na kiungo wa kati wa Italia, Marco Verratti, mwenye umri wa miaka 30 ambaye hayumo katika mipango ya kocha mpya wa PSG, Luis Enrique. **(Foot Mercato)**

### KANE NDOTO IMETIMIA

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya England, Harry Kane, amefikia makubaliano na Bayern Munich ya kuondoka Tottenham Hotspur na kujiunga na klabu ya Ujerumani kwa mkataba wa miaka minne. **(Athletic)**

### BALOGUN MAMBO BADO

KLABU ya Inter Milan haitaki kufikia thamani Arsenal kwa Folarin Balogun na imejiondoa katika mazungumzo kuhusu kumsajili mshambuliaji huyo wa Marekani mwenye umri wa miaka 22. **(Calciomercato)**

### NAPOLI KUMBAKISHA OSIMHEN

RAIS wa Napoli, Aurelio De Laurentiis, amesema mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Nigeria, Victor Osimhen, mwenye umri wa miaka 24, atasalia na mabingwa hao wa Serie A kwa msimu ujao. **(Sky Sports Italia)**

### LEEDS: GNONTO HAUZWI

EVERTON imeambiwa na Leeds United mshambuliaji wa Italia, Wilfried Gnonto, mwenye umri wa miaka 19 hauzwi na sasa wako mbioni kumsajili mshambuliaji wa Ureno Youssef Chermiti (19), kutoka Sporting Lisbon. **(Liverpool Echo)**

### PAQUETA KUIKAMUA CITY

MANCHESTER City imeambiwa lazima ilipe ada ya pauni milioni 80 ili kumsajili kiungo mshambuliaji wa Brazil, Lucas Paqueta, mwenye umri wa miaka 25 kutoka West Ham. **(Teamtalk)**

## DOND SOKA MAGAZ LAYA



# KANE RASMI NI MALI YA BAYERN MUNICH

●●● Mshambuliaji huyo sasa amehitimisha miaka 19 aliyodumu...

**LONDON, England**

MSHAMBULIAJI wa Tottenham Hotspur, Harry Kane amekubali kujiunga na Bayern Munich kwa mkataba ambao unaweza kugharimu hadi euro milioni 120, kwa mujibu wa ESPN.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 jana alitarajiwa kusafiri hadi Ujerumani kufanyiwa uchunguzi wa kimatibabu kabla ya kusaini mkataba wa miaka minne.

Hata hivyo, kulitokea hali ya sintofahamu na kucheleweshwa yeye kusafiri kuelekea huko Ujerumani.

Vyanzo viliiambia ESPN Tottenham ilitaka kujadili upya vipengele fulani vya ada ya uhamisho na Bayern Munich.

Chanzo kimoja kilisema walikuwa wakitafuta kiasi kikubwa cha malipo ya uhakika, ingawa hii haikuthibitishwa.

Vyanzo vya karibu na Tottenham viliamua kukana matatizo yoyote kuhusu uhamisho huo na kusisitiza alikuwa na ruhusa ya kwenda Ujerumani, lakini inafahamika Kane alikuwa akisubiri katika nyumba ya familia kabla ya kuruhusiwa kuondoka nchini England.

ESPN ilifichua mapema mwezi huu Bayern Munich walikuwa tayari kulipa euro milioni 100 pamoja na hadi euro milioni 20 kama nyongeza na uhamisho sasa umekubaliwa kwa bei hiyo baada ya kurekebishwa muundo wa masharti.

Uamuzi wa Kane kuondoka unahitimisha sakata la muda mrefu ambalo hatimaye linahitimisha maisha yake ya miaka 19 na Spurs.

Bayern Munich ilikataliwa ofa tatu na Ijumaa iliyopita ilikamilisha makubaliano pekee ya kuwasilisha ofa ya nne ambayo Tottenham ilikubali bila kusita, na kumwacha Kane kuamua mustakabali wake.

Vyanzo vimeiambia ESPN, nahodha huyo wa England alifikiria kwa dhati kubaki ili kuona mwaka wa mwisho wa mkataba wake baada ya kocha mkuu mpya, Ange Postecoglou, kutoa maoni chanya katika klabu hiyo lakini nia ya Kane ya kushinda mataji ndiyo sababu iliyomfanya aondoke.

Kocha wa Bayern, Thomas Tuchel alikuwa na nia ya kumleta Kane Chelsea wakati alipokuwa Stamford Bridge na ameweka shabaha yake kuu kuongoza safu ya ushambuliaji ya timu yake huku wakilenga kunyakua taji la 12 mfululizo la Bundesliga.

Kane atasalia na mabao 213 ya Ligi Kuu England, akipitwa 48 kwa rekodi ya muda wote na Alan Shearer.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,142,1
MECHI KALI
ARSENAL
VERSUS
NOTTINGHAM
1 | 1.24
X | 6.21
2 | 11.87
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# GUARDIOLA HATARAJII MAAJABU 2023/24



**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola amedai viwango vya wachezaji wa timu yake ya Manchester City vitashuka baada ya mafanikio ya msimu uliopita.

Bosi huyo wa City amekubali timu yake haitaweza kufikia kiwango kilichowafanya kutwaa mataji matatu msimu uliopita ( Ligi Kuu England, Kombe la FA na Ligi ya Mabingwa Ulaya).

"Sidhani kama tutakuwa bora kama msimu uliopita," alisema Guardiola, ambaye timu yake jana usiku ilianza harakati zake za kusaka taji la sita la Ligi Kuu England kwa kucheza dhidi ya Burnley.

"Ni lazima kidogo. Tutajaribu kuizuia iwezekanavyo. Kisha jaribu, katika miezi minne, kujaribu kufanya kile ambacho tumefanya kila msimu."

Guardiola pia hataki kuweka malengo yoyote kwa Erling Haaland katika msimu wake wa pili kwenye klabu hiyo.

Raia huyo wa Norway, alifurahia mwaka wake wa kwanza, akifunga mabao 52 katika mechi 53 pekee.

Guardiola alisema: "Nitamshauri, asiweke shinikizo kwenye mabao. Nilimwambia Erling, rudi ukiwa bora, kimwili na kiakili. Ukifunga, sawa. Ikiwa hutafunga ni sawa pia."

# Wan-Bissaka atoboa siri

**LONDON, England**

AARON Wan-Bissaka amesema alihofia maisha yake ya soka pale Manchester United yangefikia mwisho wakati akiwa nje ya timu baada ya Erik ten Hag kuteuliwa kuwa kocha mpya.

Beki huyo alikaa nje kwa miezi mitatu baada ya kuwasili kwa Ten Hag msimu uliopita wa joto na hakuanza mchezo hata mmoja kabla ya mapumziko ya Kombe la Dunia hapo Desemba mwaka jana.

Alipambana na kuwa chaguo la kwanza la beki wa kulia wa United katika kipindi cha pili cha msimu, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 alisema wakati fulani, alifikiri muda wake Old Trafford unaweza kuwa umefikia mwisho.

"Una hisia hiyo, lakini kwangu mimi huwa na imani hiyo ndani yangu ya kujiondoa katika hali kama hizo," alisema Wan-Bissaka. "Nilikuwa na kichwa changu na nilikuwa tayari kufanya kile kinachohitajika.

"Ulikuwa wakati mgumu na kitu pekee unachoweza kufanya katika wakati mgumu ni kuendelea kufanya kazi. Niliinamisha kichwa chini kisha nikapata nafasi na kuisaidia timu.

"Unaweza kukaa tu na kulalamika juu yake na usijali, au unaweza kujaribu na nilifikiri njia bora zaidi ilikuwa kwangu kujaribu."

Wan-Bissaka anachukuliwa kuwa mmoja wa mabeki bora wa mchezaji mmoja mmoja kwenye Ligi Kuu England, lakini alisema amelazimika kufanyia kazi ya ziada ili kumvutia Ten Hag na kurudisha nafasi yake kwenye timu.

Anatazamiwa kwa vita nyingine ya kuwania nafasi ya beki wa kulia msimu huu akiwa na ushindani kutoka kwa mchezaji wa kimataifa wa Ureno, Diogo Dalot.



## HABARI MICHEZO

# WANAMITINDO WANNE WAPITA MCHUJO WA FUTURE FACE 2023

**Na Mwandishi Wetu**

WANAMITINDO wanne wamepita katika mchujo wa awali ulioshirikisha warembo zaidi ya 200 ambao waliojitokeza kusaka nafasi ya kuiwakilisha Tanzania kwenye mashindano ya kimataifa ya Future Face 2023, imeelezwa.

Akizungumza wakati wa kutangaza washindi hao, Jaji Mkuu wa shindano hilo, mwanamitindo wa kimataifa wa Tanzania, Happiness Millen Magese, aliwataja wanamitindo waliopita ni Rachel Julius (20), Joyceller Lasway (25), Neema Evaresty (23) na Jasinta Makwabe (25).

"Nawashukuru majaji wote kwa ushiriki na kujitoa kwao kufanikisha jambo hili muhimu ambalo limeandika historia kubwa katika nchi yetu, hii ni mara ya kwanza kwa shindano la Future Face linafanyika Tanzania.

Pia nawashukuru sana vijana wote kwa kujitokeza kwa wingi, sikutegemea kuona umati uliojitokeza na kama mtu hakuweza kufika basi anaruhusiwa kutuma maombi yake kwa njia ya mtandao kupitia www.futurefaceglobal.com , mwisho wa kutuma ni Septemba 22, mwaka huu," alisema Magese.

Aliongeza anawataka wanamitindo hao waliopita kujipanga kuonyesha ushindani kuelekea mashindano ya kimataifa na huko wafahamu kuna kushinda au kushindwa.

Alisema mshindi ataenda kuiwakilisha nchi katika shindano la Afrika litakalofanyika Septemba mwishoni nchini Nigeria ili kusaka mwakilishi wa Afrika atakayekwenda kuchuana katika shindano la dunia litakalofanyika Paris, Ufaransa.

Aliongeza shindano hilo alishirikiana na kampuni ya Future Face kuliandaa na litakuwa likisimamiwa na wakala maarufu Afrika Beth Model Management.




# Robertinho na Gamondi wafunguka

INATOKA UK. 24

ya kesho haitakuwa rahisi kwa sababu ya ubora wa vikosi vya timu zote mbili na anakwenda kufanyia kazi safu yake ya ushambuliaji ili ipate nafasi ya kupita ngome ya ulinzi ya Simba.

"Nimewaona Simba wana timu nzuri, wachezaji pia, mechi itakuwa ya ushindani mkubwa, ukiangalia ubora wa wapinzani wetu, safu yao ya ulinzi iko vizuri tunatakiwa kuongeza umakini safu yetu ya ushambuliaji.

Nimepata taarifa juu ya hizi mechi zinakuwa na ushindani mkubwa kwa sababu ni dabi, kikubwa tunahitaji kufanya vizuri, tumerudi uwanja wa mazoezi kufanyia kazi kile tulichokiona kwa wapinzani wetu," alisema Gamondi.

Wakati huo huo, Simba imeimarisha safu yake ya lango kwa kumsajili Lakred ili kusaidiana na Salim pamoja na Hussein Abel ambaye ametua akitokea KMC FC.

Chanzo chetu kiliiambia Nipashe tayari makubaliano yamefikia katika hatua nzuri kati ya kipa huyo Mwarabu na klabu ambayo ilifikia uamuzi wa kuvunja mkataba na Jefferson Luis, kutokana na kuumia kambini Uturuki.

"Ni kweli yupo nchini na maongezi hadi sasa yanaendelea vizuri, matumaini yetu atakuwa msaada mkubwa kutokana na ushiriki wa timu katika mashindano mengi ya ndani na kimataifa, " kilisema chanzo chetu.

Kupitia ukurasa wa instagram wa Rais wa heshima wa klabu hiyo, Mohammed Dewji 'Mo Dewji' aliandika Simba inahitaji golikipa mzoefu zaidi ili kufikia malengo yake.

"Ally ni kipa mzuri na Aishi (Manula) ni Tanzania One, kuelekea mashindano ya Super League na Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba inahitaji kipa mwingine," aliandika Mo Dewji jana.

Dirisha la usajili la ndani na lile la kimataifa kwa Simba litafungwa ifikapo Agosti 31, mwaka huu.

# NBC yaimwagia mabilioni TFF

INATOKA UK. 24

kwa thamani ya chapa yetu, tunajivua hilo na ndio maana tulianzisha mazungumzo ya kuongeza udhamini wetu ambao utashuka mpaka kwenye Ligi za Vijana na ile ya Championship, tunashukuru sana na tunajivunia hilo," alisema Sabi.

NBC ilianza kudhamini Ligi Kuu Tanzania Bara kuanzia msimu wa mwaka 2021/2022.


32,257/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 13/08/23 | 13:00 | Daejeon Citizen FC vs FC Seoul | 2.75 | 3.20 | 2.27 |
| 02. 13/08/23 | 13:30 | Incheon United FC vs Daegu FC | 2.25 | 3.10 | 2.80 |
| 03. 13/08/23 | 14:00 | Naestved BK vs Kolding IF | 2.75 | 3.25 | 2.23 |
| 04. 13/08/23 | 15:15 | FC Baden vs FC Vaduz | 2.65 | 3.20 | 2.33 |
| 05. 13/08/23 | 16:00 | IK Sirius vs Kalmar FF | 2.25 | 3.15 | 2.80 |
| 06. 13/08/23 | 16:00 | Brentford FC vs Tottenham Hotspur | 2.70 | 3.45 | 2.37 |
| 07. 13/08/23 | 16:00 | FC Nantes vs Toulouse FC | 2.46 | 3.30 | 2.70 |
| 08. 13/08/23 | 16:00 | Hobro IK vs Vendsyssel FF | 2.39 | 3.25 | 2.55 |
| 09. 13/08/23 | 17:00 | Cercle Brugge vs KRC Genk | 2.80 | 3.50 | 2.28 |
| 10. 13/08/23 | 17:00 | Motherwell FC vs Hibernian FC | 2.55 | 3.25 | 2.65 |
| 11. 13/08/23 | 18:00 | Burgos CF vs SD Huesca | 2.27 | 3.05 | 3.20 |
| 12. 13/08/23 | 18:00 | FF Jaro vs HIFK Helsinki | 2.55 | 3.20 | 2.42 |
| 13. 13/08/23 | 18:30 | Halmstads BK vs IFK Norrkoping FK | 2.55 | 3.10 | 2.46 |
| 14. 13/08/23 | 18:30 | Chelsea FC vs Liverpool FC | 2.70 | 3.50 | 2.35 |
| 15. 13/08/23 | 19:15 | Erzurumspor FK vs Bandirmaspor | 2.45 | 3.30 | 2.43 |
| 16. 13/08/23 | 20:00 | Estrela Amadora vs Vitoria SC Guimaraes | 2.65 | 3.10 | 2.60 |
| 17. 13/08/23 | 20:30 | Albacete Balompie vs Espanyol Barcelona | 2.95 | 3.15 | 2.35 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 12/08/2023


| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 2046 | Coventry vs Middlesbrough | 2.39 | 3.22 | 2.77 |
| 14:30 | 3018 | Arsenal vs Nottingham | 1.24 | 6.21 | 11.87 |
| 14:30 | 3216 | Sonderjyske vs Horsens | 2.11 | 3.48 | 2.87 |
| 16:00 | 5121 | Zlin vs Slovan Liberec | 2.75 | 3.16 | 2.50 |
| 16:00 | 5938 | Nacional Madeira vs Maritimo | 2.67 | 3.33 | 2.38 |
| 16:30 | 1901 | Viktoria Koln vs Werder Bremen | 5.69 | 4.53 | 1.51 |
| 17:00 | 1137 | Ross County vs St Johnstone | 2.07 | 3.18 | 3.47 |
| 17:00 | 1451 | Millwall vs Bristol City | 1.82 | 3.40 | 4.04 |
| 17:00 | 1692 | Southampton vs Norwich City | 1.80 | 3.61 | 3.90 |
| 17:00 | 2155 | Preston vs Sunderland | 2.62 | 3.21 | 2.52 |
| 17:00 | 2436 | Ipswich vs Stoke City | 2.06 | 3.46 | 3.17 |
| 17:00 | 2459 | Sheffield Utd vs Crystal Palace | 3.04 | 3.25 | 2.42 |
| 17:00 | 2863 | Hull City vs Sheffield Wed | 2.22 | 3.31 | 2.97 |
| 17:00 | 2897 | Bristol Rovers vs Barnsley | 2.95 | 3.30 | 2.29 |
| 17:00 | 3046 | Wigan vs Northampton | 2.02 | 3.50 | 3.35 |
| 17:00 | 3692 | Cardiff vs QPR | 2.05 | 3.27 | 3.37 |
| 17:00 | 4127 | West Bromwich vs Swansea | 1.96 | 3.31 | 3.61 |
| 17:00 | 4244 | Brighton vs Luton Town | 1.34 | 5.34 | 8.42 |
| 17:00 | 4311 | Everton vs Fulham | 2.25 | 3.41 | 3.20 |
| 17:00 | 5201 | Bournemouth vs West Ham | 2.68 | 3.46 | 2.58 |
| 17:00 | 5462 | Birmingham vs Leeds | 3.64 | 3.44 | 1.91 |
| 17:00 | 5776 | Watford vs Plymouth | 1.71 | 3.56 | 4.45 |
| 17:00 | 5879 | Huddersfield vs Leicester | 4.08 | 3.60 | 1.76 |
| 17:30 | 3423 | Gazovik Orenburg vs FC Krasnodar | 2.87 | 3.49 | 2.20 |
| 17:30 | 3870 | PSV Eindhoven vs Utrecht | 1.40 | 4.53 | 6.47 |
| 18:00 | 1595 | FK Rostov W vs FC Dinamo Moscow | 2.90 | 2.55 | 2.75 |
| 18:00 | 2505 | Real Sociedad vs Girona | 1.64 | 3.95 | 5.33 |
| 18:00 | 4732 | Marseille vs Reims | 1.71 | 3.96 | 4.73 |
| 18:45 | 5702 | Empoli vs Cittadella | 1.63 | 3.59 | 5.41 |
| 19:00 | 2748 | SV Elversberg vs Mainz | 3.55 | 3.81 | 1.94 |
| 19:00 | 5207 | FC Stade LS Ouchy vs FC Zurich | 3.72 | 3.56 | 1.87 |
| 19:15 | 3816 | Kasimpasa vs Ankaragucu | 2.29 | 3.46 | 2.79 |
| 19:30 | 5910 | Newcastle vs Aston Villa | 1.79 | 3.86 | 4.32 |
| 20:00 | 2799 | Rostov vs Rubin Kazan | 2.20 | 3.14 | 3.14 |
| 20:00 | 4943 | Sporting Farense vs Casa Pia Atletico | 2.41 | 3.04 | 2.94 |
| 20:30 | 1053 | LASK Linz vs Blau Weiss Linz | 1.46 | 4.03 | 5.64 |
| 20:30 | 1601 | Las Palmas UD vs Mallorca | 2.46 | 3.03 | 3.18 |
| 20:30 | 2910 | CDA Aguilas FC vs Real Murcia | 5.40 | 3.75 | 1.50 |
| 20:30 | 3485 | CF Algeciras vs Malaga | 3.05 | 3.31 | 2.13 |
| 21:00 | 1165 | Vsnk Varazdin vs Rudes Zagreb | 1.64 | 3.52 | 4.63 |
| 21:30 | 3808 | Juventus vs Atalanta | 2.02 | 3.61 | 3.05 |
| 21:45 | 2166 | Kayserispor vs Galatasaray | 4.73 | 3.79 | 1.64 |
| 21:45 | 5819 | Bayern Munchen vs RB Leipzig | 1.60 | 3.98 | 4.46 |
| 22:00 | 1362 | Verona vs Ascoli | 1.56 | 3.80 | 5.83 |
| 22:00 | 3640 | Paris St Germain vs Lorient | 1.38 | 5.12 | 7.58 |
| 22:00 | 4846 | PEC Zwolle vs Sparta Rotterdam | 2.44 | 3.33 | 2.64 |
| 22:15 | 5073 | Cagliari vs Palermo | 1.69 | 3.70 | 4.69 |
| 22:30 | 1147 | Sporting Lisbon vs FC Vizela | 1.15 | 6.57 | 14.94 |
| 22:30 | 2903 | Athletic Bilbao vs Real Madrid | 3.19 | 3.39 | 2.26 |
| 23:00 | 4948 | Elche vs Racing Ferrol | 1.61 | 3.62 | 5.15 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumamosi Agosti 12, 2023

Nipashe

Kane rasmi ni mali ya Bayern Munich

UKURASA 21




Rais wa Shirikisho la Soka Nchini (TFF) Wallace Karia (wa tatu kushoto) sambamba na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi ( watatu kulia) wakionyesha hundi ya mfano ya Sh. bilioni 32.5 ikiwa ni udhamini wa Ligi Kuu ya Bara kutoka katika benki hiyo kwa kipindi kingine cha miaka mitano.Wengine ni viongozi waandamizi kutoka pande zote mbili. **PICHA: TFF**



# ROBERTINHO NA GAMONDI WAFUNGUKA

## ●●●Ni kuelekea fainali ya Ngao ya Jamii, Simba yashusha kipa mpya...

**Faustine Feliciane na Saada Akida, TANGA**

WAKATI Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliviera 'Robertinho' amesema anaamini soka safi litachezwa katika mechi ya fainali ya Ngao ya Jamii dhidi ya Yanga, Wekundu wa Msimbazi wamefanikiwa kumnasa golikipa mpya, Ayoub Lakred kutoka ASFAR Rabat ya Morocco, imefahamika.

Taarifa zilizopatikana jana zinasema Lakred tayari ameshatua nchini kwa ajili ya kukamilisha mchakato huo na kuimarisha kikosi cha Simba ambacho kinahitaji kufanya vizuri katika msimu mpya wa mashindano.

Simba imetinga hatua ya fainali baada ya kuifunga Singida Fountain Gate FC penalti 4-2 wakati Yanga ilitangulia kutokana na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Azam FC kwenye mchezo wa hatua ya nusu fainali ya kwanza ya michuano hiyo inayofanyika kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini hapa.

Akizungumza na Nipashe, Robertinho alisema mchezo wa juzi ulikuwa mgumu kutokana na wapinzani wao kucheza kwa kukamia hali iliyowapa wakati mgumu wakati wote.

"Kwangu mchezo ujao wa fainali dhidi ya Yanga utakuwa mzuri zaidi, kwa sababu nao wanapenda kucheza mpira, Singida walikuwa wakicheza soka la nguvu zaidi na kuwafikia wachezaji wangu kitu kilichotufanya kipindi cha kwanza tusicheze mpira wetu," alisema Robertinho.

Kocha huyo alisema licha ya uwanja wa Mkwakwani kutokuwa na ubora kama Benjamin Mkapa, bado anaamini mchezo dhidi ya watani zao, Yanga utakuwa bora zaidi.

"Simba hatuchezi mpira wa kushambulia kwa kushtukiza, tunaanzisha mashambulizi kuanzia nyuma, tunachezea mpira, nimeiona Yanga nao wanapenda kuanzia nyuma, mchezo wetu utakuwa mzuri na Simba ya Samba itaonekana," alisema kocha huyo.

Mbrazil huyo pia aliweka wazi Singida Fountain Gate imeimarika zaidi ukilinganisha na ilivyokuwa katika msimu uliopita ambapo kwa sasa inaundwa na wanachezaji wazuri wenye uwezo wa kuwasaidia kufanya vyema katika Ligi Kuu na mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika watakayoshiriki.

Pia aliwapongeza wachezaji wake kwa kuonyesha kiwango kizuri lakini sifa zaidi zikienda kwa golikipa wake, Ally Salim, ambaye alikuwa katika ubora wake.

Naye Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, ameliambia gazeti hili amewasoma Simba na kusema amebaini mapungufu na ubora wa timu hiyo hasa katika safu ya ulinzi.

Kocha huyo alisema anafahamu mechi

UKURASA. 23

# NBC yaimwagia mabilioni TFF

**Na Faustine Feliciane, TANGA**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC), imeingia mkataba na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) kwa ajili ya kuendelea kudhamini Ligi Kuu Bara kwa muda wa miaka mitano wenye thamani ya Sh. bilioni 32.6, imeelezwa jijini hapa jana.

Mkataba huo mpya kati ya TFF na NBC utamalizika ifikapo msimu wa mwaka 2027/2028.

Mkataba wa awali wa udhamini wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16 kutoka mikoa mbalimbali ambao ulikuwa na thamani ya Sh. bilioni tisa utamalizika baada ya kumalizika kwa msimu ujao wa mwaka 2023/2024.

Moja ya makubaliano yaliyoainishwa katika mkataba mpya ni NBC kudhamini pia Ligi ya Championship na Ligi ya Vijana ambazo zote zitapewa majina mapya yenye kutangaza 'brand' ya benki hiyo .

Akizungumza katika hafla fupi jana, Rais wa TFF, Wallace Karia, alisema udhamini huo mpya utaongeza thamani ya soka la Tanzania kuanzia katika Ligi Kuu Bara na Ligi ya Vijana ambazo udhamini huo utaenda kugusa.

"Udhamini huu utanufaisha ligi yetu ya championship, Ligi ya Vijana ya U-20 ambayo zamani ilikuwa inaitwa Uhai, sasa itapewa jina jipya kutoka kwa mdhamini wetu kwa sababu ana bidhaa nyingi na hatutaweza kutumia tena neo NBC, watatupa jina jingine na rasmi litakuwa linatumika hillo kwenye ligi hizi," alisema Karia.

Rais huyo alisema kutokana na maslahi yaliyopo katika mkataba huo, TFF haitaruhusu wanachama wake kutumia kwa manufaa yoyote washindani wa kibiashara wa mdhamini huyo mkuu.

"Hapa nataka kutoa msisitizo kwa wanachama wote wa TFF, hatutavumilia kuona mwanachama yoyote anaingia makubaliano na tasisi nyingine zenye ushindani na mdhamini wetu mkuu NBC, tutawachukulia hatua wale wote watakaokwenda kinyume au kuharibu chapa ya mdhamini," Karia alisema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa NBC, Theobald Sabi, alisema benki hiyo imeona manufaa katika kudhamini mpira wa Tanzania na ndio sababu ya kuingia mkataba huo mpya.

"Kupitia mpira kwenye udhamini wetu wa awali tumeona kupanda

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >